

# *BWANA, SISI*

## *TUNATAKA KUMWONA YESU*



Amini tu;  
Amini tu, amini tu,  
Mambo yote yawezekana, amini tu.

<sup>2</sup> Tunapoinamisha vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi, sijui ni wangapi hapa wangetaka kukumbukwa, kuinua tu mkono wako, na kufanya haja yako ijulikane? Vema. Hebu tuombe.

<sup>3</sup> Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya haya, majaliwa makuu tuliyo nayo ya kukutanika pamoja tena kabla ya Kuja kwa Bwana. Pia tunaomba, Baba, kwamba huku hakutakuwa tu ni kukutanika pamoja kwa kawaida, bali kutakuwa ni kukutanika Kwako, katika vifungo vya upendo Wako na ushirika. Tunaomba ya kwamba Wewe utaokoa kila mmoja anayekuja kwenye mkutano. Wajaze na Roho Mtakatifu wale ambao kwa muda mrefu wamekuwa na shauku na Huyo, Baba. Mponye kila mtu mgonjwa na anayeteseka. Jalia tukae kwa kicho na tuwe kimya, tukikungojea Wewe, na kungojea kuja kwa jibu ambalo tumeliombea kwa muda mrefu sana. Mbariki mchungaji huyu, Ndugu Vick, na Ndugu Boze na wahudumu wengine wote, rafiki zetu wote. Sasa tunajikabidhi sisi wenyewe, pamoja na jengo hili, Kwako. Katika Jina la Bwana Yesu, kwamba wakati tumekusanyika hapa, Wewe utatutumia kwa ajili ya utukufu Wako. Amina. Amina. (Ketini.)

<sup>4</sup> Ni majaliwa makubwa sana kuwa hapa. Kwa muda mrefu nilingojea wakati ninii . . . moja ya nyakati za kipekee sana za . . . Kama nilivyomwambia mchungaji, asubuhi ya leo, safari yangu ilikuwa kukutana na Ndugu Vick, na kuwa na wakati huu wa ushirika pamoja na yeye na nyinyi watu.

<sup>5</sup> Sifiki New York mara nyingi sana. Inaonekana kana kwamba ni . . . Ninaishi Tucson, Arizona, mwajua, na daima ninahudumu nje Magharibi huko. Pia tunajiandaa kuenda ng'ambo sasa, moja kwa moja, kwa karibu ziara nyingine ya ulimwenguni kote. Na kwa hiyo kujua kwamba inanibidi kuja New York kabla ya kuenda huko, hakika ninahesabu hilo kuwa ni majaliwa makubwa na baraka kutoka kwa Mungu kuwa hapa pamoja nanyi.

<sup>6</sup> Sasa, siji, kama mlivyojua awali, kuwakilisha kanisa lolote maalumu au dhehebu fulani, ama kanuni yoyote ya imani. Ninampenda tu Bwana, na mmoja wenu, kwa hiyo tupo tu hapa kumtumikia Yeye. Na sasa, nasi humtumikia Yeye kama . . .

<sup>7</sup> Unasema, “Vema, unapotuzungumzia, Ndugu Branham, sisi ni, na hiyo—hiyo inamtumikia Bwana.” Vema, kama mnavyoitikia kuamini, na pamoja tunamtumikia Bwana. Sisi wawili pamoja hufanya kitu hicho.

<sup>8</sup> Mnajua, nilikuwa nikifanya kazi kama fundi wa umeme. Na ninakuta kwamba unaweza kuwa na waya ambao una nguvu nyingi za umeme, lakini haufanyi kazi mpaka uunganishwe na ardhi. Kwa hiyo basi wakati ukiunganishwa na ardhi, ndipo unapata matokeo, nguvu za umeme. Kwa hiyo lazima tu—tuwe na sehemu zote mbili za waya, ku—kuufanya ufanye kazi vizuri.

<sup>9</sup> Na kama kungewahi kuwa na unenaji mzuri hivyo, na hata hivyo hakuna mtu wa kuamini Hilo, Hilo lisingefanya kazi. Lakini ikiwa kuna mtu wa kuamini Hilo, basi Hilo linakuwa na ufanisi kabisa. [Ndugu mmoja anasema, “Tunaamini!”—Mh.] Na sisi. . . Asante, ndugu. Hilo ni jema. Ninapenda hilo, “Tunaamini.” Hilo ndilo lililotuleta hapa.

<sup>10</sup> Na kwa kweli ninaamini kwamba tunakabiliwa tu na tukio fulani kubwa. Na—natumaini ni Kuja kwa Bwana. Kufanyika. . . Tunajua kitu fulani hakina budi kuachilia, ulimwengu uko chini ya mvutano mwingi sana. Na kuna kitu kilicho kasoro. Kila mtu anajua hilo. Na mimi—mimi ninaamini kwamba tunakaribia kitu fulani kikuu, pia ninaamini, kwa moyo wangu wote, kwamba ni Kuja kwa pili kwa Bwana Yesu. Na ninatumaini kwamba Yeye atamwaga Roho Wake juu yetu, na atatufunulia mambo ambayo tunapaswa kufanya ili kujitayarisha kwa ajili ya Kuja Kwake.

<sup>11</sup> Sasa, ninatambua, kuja hapa pamoja na Ndugu Vick, ndugu hawa, mimi. . . Ni kazi kubwa, kwa sababu kumekuwa na watu wengi mashuhuri hapa ndani, wahubiri mashuhuri wenye ushawishi. Nilikuwa nikimsikiliza Ndugu William Booth-Clibborn, wakati mmoja, akizungumzia kuwa na mkutano mrefu pamoja na Kanisa la Rock. Je! nimesema hilo vizuri? Ni Kanisa la Rock. Nami ninaliita “kanisa la jiwe,” wakati wote. Kwa hiyo yote ni Mimi. . . Na kwa hiyo, na watu wengine wengi mashuhuri ambao wamekuwa wakitembelea mahali hapa. Na mimi nimetamani kuwa pamoja na kanisa mimi mwenyewe. Na kukutana na watu. . . Au kuingia mimbarani ambapo watu wamewasikiliza watu kama hao, na mchungaji wenu, Ndugu Boze, Daktari Lee Vayle, na wengi wa hao wahudumu wengine mashuhuri, kwa—kwa namna fulani hunifanya nijisikie mdogo sana. Bali nipo hapa kufanya sehemu yangu katika hili. Labda kidole kinajisikia mdogo sana ukilinganisha na—na nia, lakini hata hivyo ha—hakina budi kubaki kidole. Unaona, lazima tu—tuwe nacho.

<sup>12</sup> Kwa hiyo sasa fungu dogo tu linalojulikana, ili tusikae muda mrefu kupita kiasi, fungu dogo ambalo kwa kawaida huwa

ninatanguliza kwa mkutano, na kila mara kujaribu kuzunguka mahali fulani tofauti.

<sup>13</sup> Tulikuwa tunaenda kuwa na mstari wa maombi, usiku wa leo, wa kuwaombea wagonjwa katika...katika m—mstari wa maombi. Na mwanangu, ambaye nilikutana na nani mpendwa...baadhi ya watu wa kanisa la jiwe, asubuhi ya leo, Kanisa la Rock, samahani. Ndugu Boze aliniambia kwamba hiyo ilikuwa kwa sababu nilitoka Magharibi, sababu ninaliita ji—jiwe; huko nje wanaliita jiwe, hapa wanauita mwamba. Kwa hiyo mimi kukutana na watu hao wazuri, na wao...tuliweka kila kitu katika utaratibu, nikasema, “Sasa nitaenda huko.” Ndipo wao wakanipatia lundo la kadi za maombi, kasema, “Chukua hizi na umpe mwanangu azisambaze, kusudi tuweze kuombea wagonjwa.” Vema, hakujua tulikuwa tunaenda kulifanya hivyo, kwa hiyo yeye na baadhi ya ndugu walikuwa wametoka na kuenda, na hawakuingia kwa wakati ufaao kusambaza kadi hizo. Lakini nadhani tayari wametangaza njia fulani watakyokuwa wakizisambaza kesho, vyovyote ilivyo, jinsi watakyokuwa wakizisambaza kesho.

<sup>14</sup> Lakini nilifikiria basi, usiku wa leo, pamoja na utangulizi mfupi wa kile tunachotaka kuzungumzia.

<sup>15</sup> Sasa, watu wengi, tukizungumzia u—uponyaji wa Kiungu au somo lolote jingine katika Biblia, kitu cha kwanza tunachopata, kizuizi kikubwa kuliko vyote, ni, watu wanajaribu kuujenga ama huko nyuma kabisa katika wakati uliopita au huko mbali katika wakati ujao, ama uko juu sana hata hakuna mtu awezaye kuufikia. Sasa huyo ni ibilisi tu anayefanya hivyo.

<sup>16</sup> Kwa sababu, Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Yeye daima anabaki Mungu. Na Yeye ni mkuu tu pamoja na watu Wake, wakati Yeye anapowapata waaminio leo hii, kama Yeye alivyowahi kuwa. Pia—pia ninaamini Neno kuwa ni Biblia hii, kuwa ndilo Neno la Mungu, kwamba tu hakuna la ziada na hakuna kupunguza. Ninajua kwamba Mungu anaweza kufanya mambo ambayo Yeye hajaandika katika Biblia, kwa sababu Yeye ni Mungu. Lakini mradi tu ninajua kwamba kile ambacho ninamwona Yeye akifanya, Yeye ameandika hapa ndani, kwamba Yeye atakifanya, basi ninajua niko sahihi, kwa njia hiyo. Na kwa hiyo Yeye...Naam, Yeye hudumisha kiasi hicho, kitanitosha mimi, kwa sababu ninaona humo ndani kwamba, “Yeye alijeruhiwa kwa makosa yangu, akachubuliwa kwa uovu wangu, adhabu ya amani yangu juu Yake, kwa mapigo Yake mimi nilipona.” Ili kwamba hiyo inamaliza safari kwangu mimi.

<sup>17</sup> Tena—tena Yeye aliahidi hilo, kwamba sisi...Yeye atatufufua kwenye siku ya mwisho, kwa hiyo tunatazamia wakati huo kuja. Watakatifu wengi wa thamani wanangojea, bila shaka, kwa ajili ya wakati huo.

<sup>18</sup> Sasa, hili, Mungu inabidi ahukumu wa—watu, ulimwengu. Tunaamini kunakuja siku ambapo Mungu atauhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo. Sasa inabidi kuwe na kigezo fulani, mahali fulani, ambacho inabidi Yeye kuhukumu kwacho.

<sup>19</sup> Vema, kwa sababu watu wengi sana leo hii wangesema, “Vema, mimi ni,” hata watu wanasema wao ni “Kristo,” na “Mimi ni Kristo,” na, “Mimi ni wa Kristo,” na, “dhehebu *hili* ni la Kristo, ama, dhehebu *hili*.” Ingekuwa kidogo inatatanisha kama hakukuwa na kigezo fulani.

<sup>20</sup> Sasa kama nikienda kuuliza watu wa Katoliki katika jengo hapa, usiku wa leo, “Je nyinyi, mnafikiri Mungu atahukumu ulimwengu kwa kitu gani?”

Wangesema, “Vema, kigezo cha kanisa Katoliki.”

<sup>21</sup> Huenda nikauliza kuhusu labda dhehebu fulani jingine. Mbona, lingesema, “Mbona, kigezo cha kanisa letu.” Huenda wasiikiri moja—moja kwa moja, bali matendo yetu yanathibitisha hiyo ndiyo tunayofikiria. Lakini basi ni kanisa gani lingekuwa sahihi? Unaona, tusingejua mahali pa kwenda. Ndipo basi si kwa kundi lolote maalumu, kanisa lolote, dhehebu lolote.

<sup>22</sup> Itakuwa ni kwa Neno Lake. Unaona, hicho ndicho kigezo. Unaona? Kwa kuwa alikuwa amesema katika Yohana, wa kwanza, Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa katikati yetu, yeye yule jana, leo, na hata milele.” Kwa hiyo *Hiki* ni kitu kimoja ambacho Yeye anaweza kuhukumu ulimwengu kwacho, ambacho sisi sote itabidi tuwajibikie, Kitabu hiki. Na kwa hiyo ninatumaini kwamba Mungu atakifungua Kitabu hiki juma hili, kwetu, katika Jumbe za kiinjalisti, na katika tafsiri ambazo Yeye atatupatia, Mwenyewe, za Neno Lake, jinsi tu ambavyo Hilo limeandikwa, na kutafsiri Hilo kwetu, na ndipo ajionyeshe Mwenyewe hai hapa pamoja na sisi, ku—ku—kufanya hilo.

<sup>23</sup> Sasa kuna mambo mengi ambayo tunaweza kusema. Na wanadamu wanaweza kusema chochote, nadhani, wanachotaka kusema. Lakini kwa Mungu kulisema, hiyo hulifanya sahihi. Na basi Mungu akilisema, na halafu anarudi na kuthibitisha kwamba Yeye alilisema, basi hakuna swali hapo, kama yote ni sawa.

<sup>24</sup> Sasa hebu tuninii, kama mnataka kwa namna fulani kufuata mafungu haya ya Kimaandiko; ninaona, ninaamini wanarekodi kanda hapa. Pia ninaamini sasa, kabla hatujasoma, kutakuwako pia. . .

<sup>25</sup> Ninapaswa kuzungumza Jumapili. Je! hiyo ni kweli, Ndugu Vick? [Ndugu Vick anasema, “Kweli.”—Mh.] Jumapili asubuhi ama Jumapili—Jumapili usiku? [“Usiku, kote katika juma.”]

Usiku, kote katika juma. [“Naam.”] Na hakuna ibada za mchana, hakuna ibada za mchana. Vema. Sasa, na ndipo tutaninii. . .

<sup>26</sup> Ni wangapi wangependa kuwa na ibada ya uponyaji, kuombea wagonjwa? Hebu tuone mikono yenu, juu kote. Loo, jamani! Ni—ni wengi, zaidi, nadhani tisini na tisa kwa mia na tisini na tisa kwa mia. Hiyo ni karibu. . . Vema, hilo ni jema. Lakini sisi ni. . .

<sup>27</sup> Sasa, uponyaji wa Kiungu si Ujumbe wote. Yesu aliweka, nafikiri walidai, yapata asilimia themani ya huduma Yake ilikuwa ni kwa uponyaji wa Kiungu. Bali kama ma—marehemu Ndugu Bosworth. . . Wengi wenu mlimjua Ndugu F. F. Bosworth, mtu mtauwa, mtakatifu. Alizoea kusema, kwamba, “Uponyaji wa Kiungu ni kama tu chambo kwenye ndoano. Kamwe humwonyeshi samaki ndoano, unamwonyesha chambo.” Na yeye. . . Na—na kwa hiyo uponyaji wa Kiungu ni jambo la chini. Na kamwe huwezi kulifanya kuu jambo la chini, bali huelekeza kwenye lile kuu. Kwa hiyo, tu—tunaona hili.

<sup>28</sup> Nayo Biblia ni kweli, kila Neno. Na mimi ninahisi kwamba tunaweza kuning'iniza nafsi yetu juu ya Neno lolote la Biblia. Ni Neno la Mungu, na huenda mimi nisiwe na imani ya kutosha kulifanya lote litende kazi, bali kwa hakika ninaamini kwamba linaweza kufanywa, kama tuna imani ya kutosha kuliadini. Naam, kama wangeliamini.

<sup>29</sup> Sasa katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu 12:20. Wengi wenu ambao mmekuwa katika mikutano hapo kabla, hili litakuwa fungu linalojulikana sana, kwa sababu mimi hilitumia kama fungu la ufunguzi kutanguliza kile ninachotaka kusema kote katika juma, na kile ambacho tunataka kuwa tukizungumzia, na halafu Waebrania 13:8. Katika Yohana Mtakatifu 12:20.

*Basi palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu.*

*Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwomba, wakisema, Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.*

<sup>30</sup> Na mimi ninataka kuchukua tu maneno matano kutoka kwa hilo. *Bwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu.* Na kisha kwenye Waebrania 13:8.

*Yeye ni yule yule jana, . . . leo, na hata milele.*

<sup>31</sup> Sasa kama Yeye ni yule yule, na, mioyo yetu usiku wa leo, nina hakika kwamba ninazungumzia wachache mno katika mkutano huu, kwamba mioyo yetu ina njaa ya kutaka kumwona Yesu Kristo kama tu wale Wayunani walivyokuwa. Sisi. . . Hakuna mtu anayeweza kusikia habari Zake, ambaye hangetaka ku—kumwona Yeye. Imekuwa ni shauku ya moyo wangu kujua uhalisia.

<sup>32</sup> Na kwa kuwa na ujuzi m—m—mpana kwa namna fulani inafidia kidogo kukosa kwangu elimu, kwa kushughulika na dini zingine, kama vile Buddha, na—na Uislamu, na aina mbalimbali za dini. Nimeziona kote na kote ulimwenguni, ninaposafiri, na kuziangalia na kuzichunguza. Bali kuna moja tu ya Kweli ambayo ninaamini ni sahihi, hiyo ni hii, Ukristo, unaona, na halafu ndiyo—ndiyo ya pekee ambayo inaweza kuthibitisha kwamba Mwanzilishi wa dini hii hajafa. Sasa mimi. . .

<sup>33</sup> Wanabeba, wanaye farasi ameketi kwenye... ama amesimama, hasa, kwenye kaburi la Mohammed, na wao wanaamini siku moja atafufuka na kuzunguka ulimwengu wote katika ushindi. Pia, lakini amekufa. Amekuwa mfu mamia kadhaa ya miaka. Buddha alikufa yapata miaka elfu mbili mia tatu iliyopita, alikuwa ni mwanafalsafa huko—huko Japan, Uchina.

<sup>34</sup> Lakini sasa dini yetu, ya Kristo, Yeye kweli alikufa, Yeye ilibidi afe ili kwamba atuokoe. Lakini sisi tunaonyesha kaburi tupu. Na sasa Uhai Wake, ukiakisiwa ndani yetu, huthibitisha kwamba Yeye hajafa, unaona, na—na ahadi Zake.

<sup>35</sup> Sasa, bila shaka, kama ungesema hilo katika taifa geni, miongoni mwa Waislamu, wangesema, “Naam, yeye huakisi uhai wake ndani yetu. Lakini yeye kamwe hakutoa ahadi yoyote, unaona, ahadi hizi.” Bali alisema, “Yesu wenu alitoa ahadi hizi, sasa tunangojea kuona nyinyi walimu mkifanya yale Yeye aliyosema kwamba Yeye aliahidi.” Unaona, hicho ndicho kinachongojewa.

<sup>36</sup> Na hapo ndipo wao walipomshika Ndugu yetu Billy Graham, yule mwalimu wa Kiislamu, vema, kuhusu, kasema, “Kama hii . . . Wewe walete tu kiasi fulani, na mimi nitaleta kiasi fulani, na nitafanya nao kama tu utakavyofanya wewe.”

<sup>37</sup> Vema, huo ulikuwa usai kwelikweli. Lakini yeye atasai hiyo kwa mtu tofauti siku moja na ndipo, unaona, itakuwa. Sasa, ninge—ningeamini kwamba—kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

<sup>38</sup> Sasa, kulingana na Maandiko, tunapaswa kuwa “nyaraka zilizoandikwa” kumhusu Yeye. Biblia inasema kwamba sisi ni “nyaraka zilizoandikwa.” Na ikiwa, usiku wa leo, tungekuwa na njaa na kiu ya kumwona Bwana Yesu Kristo, sisi kama Wakristo waaminio tunapaswa kuakisi Maisha Yake, sana, mpaka ingekuwa mwakilishi Wake mkamilifu. Tunapaswa kuwa hilo. Kila Mkristo anapaswa kuwakilisha na kuakisi Maisha ya Yesu Kristo. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Na mimi ninaamini kwamba kila Mkristo anapaswa kuwa anaakisi Maisha ya Kristo. Alisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo naye atazifanya pia.” Na ndipo tunajua kwamba hilo ni kweli, kwamba sisi ni wawakilishi Wake. Na kama tunadai kwamba

Kristo anaishi ndani yetu, na ikiwa Kristo anaishi ndani yetu, basi tunapaswa kufanya kama Kristo alivyofanya. Tunapaswa kuakisi Maisha Yake.

<sup>39</sup> Vipi kama nilisema, usiku wa leo, kwamba ninii—kwamba uhai wa Shakes-. . . Vipi kama nilisema Shakespeare aliishi ndani yangu, ama wewe ulisema Shakespeare aliishi ndani yako? Vema, ungeandika mashairi ambayo Shakespeare aliandika, kwa sababu Shakespeare anaishi ndani yako. Vipi kama ulisema Beethoven aliishi ndani yako? Ungekuwa mtunzi mashuhuri ambaye Beethoven alikuwa, kwa sababu Beethoven anaishi ndani yako. Wewe si nafsi yako, sasa wewe ni Beethoven ama wewe ni Shakespeare.

<sup>40</sup> Basi ikiwa Kristo anaishi ndani yako, haya basi, unaona, Maisha ya Kristo unaishi. Unaona, ni hivyo tu, kama Yeye anaishi ndani yako. Bali huwezi kuishi humo ndani pamoja na Yeye; Yeye hana budi kuishi ndani yako. Hiyo ni kila mara, Yeye huchukua mahali pako, na sisi tunapaswa kumwakilisha Yeye katika kila njia.

<sup>41</sup> Sasa tunaona kwamba kanisa la kwanza lilimwakilisha Yeye, kama nyaraka zilizoandikwa, Uhai Wake uliishi kupitia watu hao. Siwezi kulinganisha kanisa letu leo hii. Kama—kama ilivyo vigumu kusema hili, kadiri ninavyopenda watu, hata hivyo inakubidi kuwa mkweli na kusema Kweli. Siwezi kusema kwamba tunaona, katika makanisa leo hii, wakimwakisi Kristo katika njia ambayo wale watu walimwakisi.

<sup>42</sup> Wao, wao walijua kuwa hao walishakuwa na Yesu. Tunaona katika mtakatifu. . . La, ninaamini ni katika Matendo mlango wa 4, ambapo tunaona, kwamba wale wavuvi, Petro na Yohana, na kumponya mtu yule kwenye Lango Zuri, na waliweza kujibu swali lolote ambalo wao—ambalo wao. . . Sanhedrin ililowauliza, ililowauliza; hata hivyo, wao pamoja na ujinga wao, na bila ya elimu. Wangeweza kutambua hilo. Hawakuwa na elimu, na wao hawakuwa wahudumu waliofunzwa, walikuwa wavuvi. “Bali walitambua kwamba walishakuwa na Yesu,” unaona, kwa sababu kwamba walikuwa wanatenda njia ile ile Yeye alitenda juu yao.

<sup>43</sup> Unaweza tu kuishi na mtu muda mrefu sana, na karibu na wao, mpaka unachukua njia zao. Na inafaa sisi tusikimbie nje na kuishi pamoja na ulimwengu. Bali tukae pamoja na Yesu mpaka tunaweza kuakisi, Maisha Yake yaakisiwe ndani ya maisha yetu.

<sup>44</sup> Na hivyo ndivyo hao wanafunzi walivyokuwa. Wao, wao walijua kwamba walishakuwa karibu na Yesu, kwa sababu waliongea kama Yeye, wakatenda kama Yeye, na kuponya kama Yeye, na kila jibu lilikuwa kama Yeye. Walivuviwa kama Yeye, na wao walijua kwamba Yeye alikuwa anaishi ndani yao. Hilo ndilo tunalopaswa kuwa wakati wote, kama waaminio. Wao

wakitenda kama Yeye, maana, kama ukishirikiana na mtu muda mrefu sana.

<sup>45</sup> Tunaona katika Biblia, kule katika Kitabu cha Wafalme, kwamba kulikuwa na mtu jina lake Yehoshafati, mtu mwenye haki. Na kulikuwa na mwana wa Ahabu, Yehoramu, na yeye alikuwa akizichukua tabia za baba yake, na halafu mfalme wa Edomu. Ndipo basi walitangaza vita, Wamoabu walitangaza, juu ya Israeli kwenye wakati huo. Na Yehoramu akiwa ni mfalme, baada ya baba yake, mbona, alimwita Yehoshafati. Na Yehoshafati, mtu mwenye haki, hakupaswa kamwe kujiunganisha na mtu huyu asiye haki. Lakini mara nyingi Wakristo hufanya hivyo, bila tu kufikiria.

<sup>46</sup> Na kwa hiyo walichukua dira ya siku saba na kuingia nyi—nyikani, ndipo, wakaja kugundua, walikuwa wameishiwa na maji. Ndipo mmoja wao akalia, “Ole, kwa sababu Mungu amewaleta wafalme hawa hapa nje kuwaua!”

<sup>47</sup> Bali Yehoshafati, akiwa ni mtu mwenye haki, katika wakati wa shida, alikumbuka kwamba Mungu angali aliishi. Unaona, haijalishi ninii. . . Ingawa tulienda kando na kufanya kosa, hata hivyo Mungu angali pamoja nasi. Mungu angali anabaki yule yule. Basi Yehoshafati, akikumbuka hili, alilia kwa sauti, “Hivi hakuna nabii wa Bwana mahali fulani, ambaye tungeweza kumtaka shauri?”

<sup>48</sup> Ndipo mmoja wa watumishi wa mfalme wa Israeli, akajibu akasema, “Naam, huyu hapa Elisha. Alimimina maji juu ya mikono ya Eliya.”

Naye Yehoshafati akasema, “Neno la Bwana liko pamoja naye.”

<sup>49</sup> Kwa nini? Angalia ushirikiano wake. Unaona, yeye, walijua mtu huyu alikuwa ameshirikiana na nabii halisi. Pia walijua kwamba ulikuwa na ushirika wa namna hiyo. Na kukaa katika ushirika wa namna hiyo, ilibidi atembe maisha yaliyonyoka kabisa, na yeye asingeweza kusema chochote. . . kwa sababu alikuwa amelelewa chini ya ualimu wa nabii huyu mashuhuri, Eliya.

<sup>50</sup> Loo, jinsi lingeweza kuwa leo hii kama kanisa lingaliweza tu kudumu na Kristo, chini ya ualimu wa Roho Mtakatifu, wasiliache Neno hilo kamwe kwa ajili ya kanuni yoyote ya imani wala chochote, waamini Hilo jinsi tu Hilo lilivyoandikwa. Na watu kila mahali wangejua kwamba wewe ulishakuwa pamoja na Yesu, pia. Hivyo ndivyo angalijua hilo.

<sup>51</sup> Lakini, leo hii, ni vibaya sana. Kwa namna fulani tunatazamia msomi aliyeelimika vizuri au kitu fulani. Huyu ndiye tunadhania tunampata Kristo ndani yake. Tunaenda kwenye shule. Tunawapeleka wavulana wetu, na kuondoka kwenda shuleni, kwenye seminari; ambalo ni sawa, bali, tunapata, wanajifunza jinsi ya kutoa hotuba zenye ufasaha,

na wanafanya mazungumzo mashuhuri. Tena—tena wao ni watu wazuri, hapana shaka, na maelfu ya hao. Na wanajua jinsi ya kuendesha ratiba. Wanajua jinsi ya kusimama jukwaani, wanajua jinsi ya—ya kumtambulisha Kristo kwa watu. Lakini unakuja kugundua, mengi ya hayo, wingi wake, mengi kabisa ya hayo, ni mtu huyo tu; sio hasa kuwa mwakilishi wa Kristo, bali mtoa hotuba. Unaona, anajua, amefunzwa ili kutoa hotuba. Ungeweza kumwuliza kutoa ho—hotuba ambayo kwa kweli ingewashtua watu, kutokana na ufasaha wake wa hotuba na jinsi angeweza kujishikilia, na jinsi ambavyo angewafanya watu kuduwaa. Na, bali tunakuta kwamba, alijifunza hayo katika seminari mahali fulani, mahali fulani ambapo walimfunza jinsi ya kufanya hivyo.

<sup>52</sup> Jinsi ilivyokuwa tofauti na Mtakatifu Paulo, wakati aliposema, “Sikuja kwenu na ufasaha wa maneno au na hekima ya ulimwenguni, bali katika nguvu za Roho Mtakatifu; ili imani yenu isiwe katika hekima ya mwanadamu na uungwana wake, bali katika ngu—nguvu za Roho Mtakatifu.”

<sup>53</sup> Naam, tunalo kundi jingine ambalo sisi kwa namna fulani, watu wengi, wanatazamia, ni jamaa tunayemwita mtu mzuri. Yeye husimama jukwaani, yeye ni mchekeshaji hodari. Anaweza kutoa mizaha michache na kuwafanya watu wote wacheke, na watu watalundikana nje kila mahali kusikia mizaha hiyo. Na labda si mizaha mibaya, ni mizaha tu inayotamkwa kutoka jukwaani, bali si—sidhani hiyo ni sahihi. Sasa mimi—mimi... hapa si mahali pa kutolea mizaha.

<sup>54</sup> Hapa ni mahali pa unyofu wa kilindi. Hiyo ndiyo shida ya kanisa leo hii, tunaenda mbali na huo unyofu wa kilindi. Inatubidi kuwa chini kabisa, wanyofu katika hili, unaona. Na halafu, Mungu anapenda unyofu, na sisi hatuwi wanyofu vya kutosha na hilo.

<sup>55</sup> Lakini tunakuta kwamba, mtu huyu anaweza kufanya kila mtu acheke na kuendelea, na kwa namna fulani tunamtazamia mtu huyo. Lakini, kwangu mimi, anaitwa, kwangu mimi, labda “mtumbuizaji,” ama labda kwa urahisi tu “mchekeshaji mimbarani,” hayo tu, unaona, kusimama hapo na—na kuwafanya tu watu wacheke. Wakati, wanapaswa kuwa, katika—katika Kuja kwa Bwana, katika kilindi cha unyofu, wakitazamia kila dakika kwa ajili ya kuonekana Kwake, kwa kuwa hatujui ni wakati gani Yeye huenda akatokea. Kwa hiyo, hatuhitaji watoa hotuba, hatuhitaji watumbuizaji, na kadhalika.

<sup>56</sup> Halafu kuna tabaka jingine la watu, wanaomtafuta Mungu, kama walikuwa wakimtafuta Yeye, katika nguo ya mtu. Watu wengi wanamwona mtu akiteremka chini mtaani akiwa na ninii fulani mashuhuri... amevalia namna fulani ya kofia ya kidini, na—na nguo za kidini zimening’inia chini, na—na, wao, wao wanafikiria kwamba huyo ni wa kidini sana, huyo anafanana

na Kristo. Na mimi sidhani hivyo. Kama hiyo ingekuwa hivyo, basi... Kristo hakuvalia namna hiyo, kwa hiyo si katika nguo. “Ufalme wa Mungu si katika chakula na mavazi, bali ni uvumilivu katika Roho Mtakatifu.”

<sup>57</sup> Wanatazamia watu, wengi wao, wanatazamia watu, watu wanamtafuta Kristo, hasa, miongoni mwa jamaa zao. Unasema, “Mama yangu, amekuwa mfuasi *fulani-fulani* wa kanisa *fulani-fulani* kwa miaka mingi sana, ama baba yangu alikuja juu.” Na wao wanamtafuta Kristo miongoni mwa watu wao namna hiyo. “Familia yangu ilinilea kuwa *hiki-na-kile*.” Lakini hatumwoni Kristo, unaona, hatuoni Hilo.

<sup>58</sup> Mnajua, Mariamu na Yusufu walifanya kosa hilo, wakati mmoja. Walikuwa watu wema. Bali walienda huko juu Yerusalemu kwenye karamu, basi njiani mwao wakirudi walimkosa Yesu miongoni mwao. Na kwa hiyo walimtafuta Yeye miongoni mwa watu wao, lakini Yeye hakupatikana. Nami ninafikiri hiyo ni kwa wingi sana, leo hii. Nao walienda kujaribu kutafuta mahali Yeye alipokuwa. Hivi ulijua mahali walipompata Yeye? Moja kwa moja mahali walipomwacha. Hiyo ni kweli.

<sup>59</sup> Vema, hapo ndipo sisi tutakapompata Yeye. Hapo ndipo kanisa litakapompata Yeye. Hatutampata Yeye katika hotuba. Hatutampata Yeye katika watumbuizaji. Hatutampata Yeye katika njia tunayovalia, ama dhehebu tunaloshiriki. Tutarudi nyuma kwenye Siku ya Pentekoste, mahali Yeye alipoingia kanisani, na hapo ndipo tutakapompata Yeye. Kwa sababu, hapo ndipo kanisa la mwanzoni lilipomwacha Yeye, na kwenye Baraza la Nikea, na hapo ndipo Yeye amekuwa ameachwa tangu wakati huo. Kwa hiyo, ni, inatubidi kurudi kwenye wakati huo, kumpata Yeye. Turudi nyuma mahali tulipomwacha Yeye, mahali ambapo tunaweza kuchukua Neno Lake; na kutoongeza chochote Kwake, kuondoa chochote Kwake. Kuliamini Hilo tu jinsi Hilo lilivyo. Hiyo ndiyo—hiyo ndiyo njia ambayo Hilo limeandikwa, hiyo ndiyo Hilo liliyo. Mungu amelitunza Hilo, kulidumisha Hilo hivi, na hicho ndicho kigezo ambacho tutahukumiwa kwacho.

<sup>60</sup> Sasa Wayunani hawa hawakuwa wakimtafuta mhadhiri, juu ya Yesu Kristo. Hawakuwa wakitafuta wachekeshaji mimbarani, kama nilivyosema dakika chache zilizopita. Hawatafuti hilo. Hawatafuti wenye kutumbuiza. Walitaka kumwona Yeye, Mtu, Yesu Kristo. Walitamani kumwona Yeye, kwa sababu walikuwa wamesikia habari Zake. “Na imani huja kwa kusikia, kusikia Neno.” Na Yeye ni Neno. Unaona, Yeye ni Neno. Unaona? Nao walitaka kumwona Yesu.

<sup>61</sup> Sasa, kamwe hawakusema kwamba walitaka kumsikia Yeye; walikuwa tayari wamesikia. Walitaka kuona. Hilo halikuwa ndilo swali, “Sisi tunataka kumsikia Yesu. Mabwana, tunataka, sisi,” wanataka, ama, “kumsikia Yesu.” Walitaka kumwona

Yesu. Hilo lilikuwa ndilo kusudi lao kuuliza, lilikuwa ni kumwona Yeye.

<sup>62</sup> Si kwamba Yeye afafanuliwe. Leo hii, kwa jumbe kuu za kiakili, tunaweza kufafanua Hilo mpaka unaweza kuiona picha. Lakini, hiyo, hiyo siyo kile tunachotafuta usiku wa leo. Hatu—hatutafuti mitambo, tunatafuta nguvu Zake. Jambo ndilo hilo. Wengi sana, unaona, ambao ni... Tunayo mitambo ya dini za Biblia imetiwa kwenye chupa sana, inaonekana kama gari moshi kubwa mashuhuri lenye mabehewa kumi na sita ama thelathini na tano lililowekwa hapa nje kwenye reli. Lakini ikiwa huna mvuke wowote ndani yake, basi ninii—ninii... Inahitaji nguvu ku—ku—kufanya kazi pamoja na mitambo. Pia kile tunachohitaji sasa ni kuona Hizo. Hiki ambacho tumefundishwa miaka hii yote, ni Kweli au si kweli? Imefafanuliwa, tena na tena na tena, kupitia seminari mbalimbali na makanisa, na kadhalika, mpaka tunatazamia kuona kuwa ni Nani Mtu huyu.

Sasa unasema, “Ndugu Branham, ungefanyaje hilo?”

<sup>63</sup> Vema, hivi ulitambua walikuja kwa mtumishi wa Kristo, ambaye alikuwa amefunzwa kujua la kufanya. Sio tu kusema, “Keti chini. Sema, ngoja sasa! Wewe keti chini hapa, nitalieleza.” La, yeye aliwaleta moja kwa moja Kwake, maana hicho ndicho walichotaka kuona. Wao, wao walisema, “Tunataka kumwona Yesu.” Sio, “Tungetaka wewe utufafanulie Hilo na utuambie kwamba Hilo lote linahusu nini.” Hilo halikuwa ndilo swali. Lakini wao walitaka kumwona Yesu. Ndipo wao... Mungu alikuwa na mtu aliyekuwa amesimama hapo, Filipo, ambaye angeweza kuwachukua na kuwaonyesha Mtu huyo, Yesu Kristo.

<sup>64</sup> Sasa hilo ndilo tunalotaka kuona. Tunataka kumwona Mtu huyo. Unasema, “Vema, Ndugu Branham, tutamwona wakati Yeye atakapokuja.” Naam, bali Yeye aliahidi kwamba Yeye, katika Utu wa Roho Mtakatifu, angekuja katika siku za mwisho na angekuwa pamoja nasi, hata ndani yetu, hadi mwisho wa ulimwengu. Na mambo aliyofanya Yeye, sisi tungefanyia pia. Alisema, katika Waebrania 13:8, kama ambavyo nimenukuu hilo, “Yeye ni—yeye yule jana, leo, na hata milele.” Sasa kungekuwa tu na njia moja ya kujua kile Yeye alichio leo.

<sup>65</sup> Tunaona tusingeweza kumpata Yeye katika hotuba nzurinzuri, maana tunakuta watu ambao wanaweza kusimama na wanaweza kufafanua Neno kwa njia hivi kwamba, inakata tu pumzi. Lakini tunapoipata, ingali ni hotuba tu. Unaona, hotuba tu, ni mitambo. Na tunamkuta mtumbuizaji ambaye anaweza kupitia matendo yote, na kadhalika, lakini hilo bado silo. Sisi, hilo silo ambalo tunatafuta. Tunakuta aina ya kidini, wakiwa wamevalia majoho yao, na kadhalika, hilo bado si kile tunachotafuta. Unaona? La.

<sup>66</sup> Tunamtafuta Mtu yule, Yesu Kristo. Unaona, Mtu yule, Yesu Kristo! Sasa, kama Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo,

na hata milele,” basi Yeye hana budi kuwa hilo, ama Biblia ilisema kitu kisicho kweli. Basi, siamini Mungu angeuhukumu ulimwengu kwa chochote kisicho sahihi.

<sup>67</sup> Basi tuko wapi tena? Unaona, sote tuko nje kwenye machafuko tena, kwa sababu kuna kila kitu, kanisa *hili* linasema, “*sisi tuna Hilo*,” na, “*sisi tuna Hilo*,” na, “*sisi tuna Hilo*,” na kadhalika. Lakini ikiwa una Hilo, ungeonyesha Hilo, hiyo ni kweli, unaona, Mtu, Kristo Yesu.

<sup>68</sup> Sasa njia ya pekee ya kweli kuona kile Yeye alichokuwa, unaona, kwa sababu Yeye habadiliki. Mungu hawezi kubadilika kamwe. Hajawahi kubadilika. “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Yeye lazima adumu vile vile. Neno Lake lazima libaki lile lile. Mipango Yake lazima ibaki ile ile.

<sup>69</sup> Sasa tumejaribu kila kitu ulimwenguni, kwenda nacho, kuachana na mipango Yake. Lakini ingali inabaki, Yake ndiyo njia pekee. Wanadamu wamejaribu kufanya njia kuwaelimisha wanadamu kwa ushirika; imeshindwa. Tumejaribu kuwaundia dhehebu ili kuwashirikisha; imeshindwa. Mungu anapo mahali pamoja ambapo Yeye hukutana na wanadamu, hapo ni chini ya Damu. Na nje ya hiyo. . . Hakuna kushindwa. Hiyo ni kweli. Inakubidi, lazima uwe, chini ya Damu.

<sup>70</sup> Sasa, kama kasisi wa Katoliki, Myahudi wa Kiothodoksi, na Mnazarayo, na Mpilgrim Holiness, na Mpentekoste, wanaweza kusimama hapa nje katika madhehebu yao na kuzozana mmoja na mwenzake, siku nzima, na kudai jinsi kila mmoja alivyo mashuhuri zaidi, na kadhalika; lakini acha wote waje chini ya hiyo Damu na kupiga magoti chini ya msalaba, wanakumbatiana mmoja na mwenzake, na wao ni ndugu kwa sababu wana—wana vitu shirika. Na hilo ni jambo moja ambalo kila mwaminio aliyezaliwa tena analo shirika, ni Damu ya Yesu Kristo ambayo huwatakasaa.

<sup>71</sup> Hadithi fupi, hapa si muda mrefu uliopita, ya fa—familia fulani, maskini familia yenye upendo ilikuwa inavunjika. Mtu na mke wake walitofautiana, na walikuwa wanaenda kuwa na talaka. Naye wakili akawaambia, kasema, “Sasa, ikiwa hamtaki mahakama kwa namna fulani zichukue kila kitu mlichu nacho, mnapaswa kushuka huko chini, na kati yenu, na mgawane ma—mali, kutoka kwa familia yenu, muungano wenu.”

<sup>72</sup> Kwa hiyo wanateremka chini kule nyumbani, na wakakutana kwenye siku fulani. Waliingia sebuleni, na wakazozana na kuhangaika juu ya kila kitu kilichokuwepo sebuleni. Ndipo wakaingia jikoni, na wakazozana na kuhangaika kuhusu kile kilichokuwa humo ndani, na vyumba tofautitofauti vya nyumba. Baada ya kitambo, waliamua kwenda juu darini, kwa sababu walikuwa na kasha la kale huko juu. Walikuwa na baadhi ya maskini vitu vya kale, ambavyo

vilikuwa vimewekwa kando, kwa hiyo walipanda darini kuvuta kasha hili. Na, wao, mmoja angesema, “*Hiki ni changu,*” “*hiki ni changu,*” na wangebishana juu yake.

<sup>73</sup> Katika dakika chache, walifunua kitu fulani, na wote wakakiendea, ndipo mikono yao ikapitana. Ilikuwa ni maskini jozi ya viatu vya mtoto, ambaye Mungu alikuwa ameipa ndoa yao, na alikuwa amemchukua kutoka kwao. Hapo, ni nani angeweza kuvidai? Kilikuwa ni kitu walichokuwa nacho shirika. Unaona? Na huku machozi yakiwa machoni mwa kila mmoja, walivuta maskini viatu hivyo katikati yao. Talaka ilifutiliwa mbali. Unaona, walipata kitu fulani ambacho kilimaanisha kitu fulani kwao wote wawili.

<sup>74</sup> Na mimi ninafikiri kwamba Ukristo unapaswa kufanya jambo lilo hilo. Tunaweza kupata kitu fulani ambacho kina maana kwetu sote wawili, hicho ni Kristo. Unaona? Hicho kinamaanisha kwetu sote, hapo tunaweza kushikana mkono mmoja na mwenzake na kusimama hapo kama ndugu na dada katika Kristo. Yeye ni Kristo. Sasa je! Yeye yu hai? Hakika yu hai, “Yu hai milele! Na kwa sababu mimi ninaishi, mnaishi pia.”

<sup>75</sup> Sasa ingetubidi kurudi nyuma, kuangalia. Tunajua tusingempata Yeye kama—kama mwe—mwelimishaji mashuhuri. Hata hatuna kumbukumbu yoyote Yake kuwahi kuenda shule. Na sisi... Yeye asingekuwa ni mtu aliyevikwa tofauti, kwa sababu Yeye aliingia na kutoka watu, miongoni mwa watu, hasa, na kamwe... Mbona, watu hawakumjua Yeye, wote walivalia sawa. Yeye hakuvalia kama kuhani. Hakuvalia kama mtu wa kidini. Alivalia tu kama mtu wa kawaida. Na—na ndipo kwa ajili ya ninii Yake... .

<sup>76</sup> Tunakuta kwamba Biblia iliandikwa katika lugha ya kawaida sana, Yeye hapana shaka alitumia sarufi ambayo ilitumiwa mtaani, watu wa kawaida tu. Kwa sababu, Biblia ilisema, “Watu wa kawaida walimsikia Yeye kwa furaha,” unaona, kwa hiyo labda wenye elimu wasingeweza kujishirikisha wenyewe katika Mtu wa kawaida namna hiyo ambaye alizungumza kwa kukokoteza maneno, na kadhalika, ambalo labda Yeye alifanya. Kwa hiyo, kidogo iliwazidi. Ingali hivyo, leo hii.

<sup>77</sup> Na hiyo ndiyo sababu Biblia ikawa shi—shida sana kwa watu, kwa sababu, ni, wanajaribu kuifasiri Hiyo kwa aina ya lugha ya kiwango cha juu, wakati Hiyo iliandikwa katika lugha ya mtaani, unaona. Ninii... .

<sup>78</sup> Kwa hiyo, Mungu hujinyenyekeza Mwenyewe. Mungu ni unyenyekevu. “Mtu anayeweza kujinyenyekeza mwenyewe yuko njiani mwake akienda juu. Yeye ajikwezaye yuko njiani mwake kushuka,” daima. Kwa hiyo lazima tukumbuke kwamba Ukristo si kujisukuma mbele, na kujaribu kuwa mbele ya jamaa *huyu*, bali kurudi nyuma na kuchukua kiketi cha nyuma, unaona,

kumwacha jamaa huyo mwingine aendeleo, huo ni—huo ni Ukristo. Jinyenyekeze. “Wakikushtaki kwenye mahakama, na kuchukua koti lako, mpe na joho pia. Akikushurutisha kwenda maili moja, enda mbili. Akikupiga shavu moja, geuza jingine.” Yeye alikuwa mfano wetu katika kila njia kile tunachopaswa kuwa. Na kama Maisha hayo yanaweza kuakisiwa ndani yetu, watu wataona Kristo ndani yako, unaona, wakati—wakati wanapoweza kuona huo.

<sup>79</sup> Vema, sasa hebu tuone, huenda kulikuwa na watu wengi. Yesu alikuwa tofauti na watu wote. Huenda kulikuwa na watu wengi ambao wangeweza kuwa wanyenyekevu, na kuenda maili ya pili, ama kugeuza shavu jingine, lakini tunaona kwamba Yesu alikuwa ni Mtu tofauti.

<sup>80</sup> Sasa, Mungu daima amedumu na Neno Lake. Kumbukeni, Yeye kamwe habadilishi Neno Lake.

<sup>81</sup> Kama nilivyosema, dakika chache zilizopita, kuhusu damu. Katika bustani ya Edeni, wakati Adamu na Hawa walipokuwa wametenda dhambi, na Mungu ilibidi atimize sheria Yake kwa sababu Yeye alikuwa mwenye haki. Na adhabu ya sheria ilikuwa, vema, ilimbidi Yeye kuweka juu ya familia hiyo, kwa sababu, “Mshahara wa dhambi ni mauti, na nyinyi mnaenda kufa.” Lakini basi walipofanyika namna fulani ya kitu fulani, Yeye angekuwa na tangazo la ukombozi. Yeye—Yeye aliamua kwamba ilihitaji damu. Adamu na Hawa walijaribu kutengeneza vazi la jani la mti; lisingefanya kazi. Kwa hiyo, Yeye alihitaji damu.

<sup>82</sup> Na Yeye kamwe hajabadilika. Kamwe habadiliki. Sasa ulipowadia wakati mtu alikuwa mgonjwa na alihitaji kuponywa na Mungu, Mungu alimponya juu ya msingi wa imani yake katika Yeye. Kamwe hajaibadilisha. Ingali vile vile, vile vile tu.

<sup>83</sup> Na Neno lolote asemalo Mungu, Hilo haliwezi kubadilishwa kamwe. Sasa hiyo ndiyo sababu ninaamini Biblia iko tu jinsi Hiyo ilivyoandikwa. Unaona, Hiyo haiwezi kubadilika kamwe. Hatuwezi kupata chochote bora; Mungu hawezi. Yeye hana kikomo. Sisi tuna kikomo. Sisi hufanya makosa, na kesho tunajua zaidi ya tuliyojua leo. Bali si Mungu; Yeye ni—Yeye ni yule wa Milele, na asiye na kikomo, mwenye nguvu zote, aliyepo kila mahali, anayejua yote. Yeye, Yeye ninii tu. . . Yeye ni Mungu. Kama Yeye si vitu hivyo, basi Yeye si Mungu, unaona, Yeye ana kikomo kama sisi tulivyo. Kwa hiyo lazima tukumbuke kwamba Yeye ni Mungu, na Maneno Yake ni hivyo, ambayo ni sehemu Yake. Mmewasikia wao wakisema, “Kila mtu ni mzuri tu kama neno lake.” Hiyo ni kweli. Mungu si bora kuliko Neno Lake.

<sup>84</sup> Yesu daima alirejea nyuma kwenye Neno la Baba, daima, kila wakati. “Imeandikwa. Imeandikwa.” Hivyo ndivyo Yeye alivyomshinda Shetani, juu ya Neno. “Imeandikwa.” Sasa tunamkuta Yeye wakati Yeye alipokuwa. . .

<sup>85</sup> Alikuwa katika uwezo wa Maandiko, hasa kabisa tafsiri ya Maandiko. Lakini watu wa siku hiyo, waliokuwa wakimtazamia Yeye kuja, walimkosa, kwa sababu walikuwa na tafsiri, hata wasingeweza kuondoka kutoka kwenye tafsiri hiyo. Hawana budi kuwa nayo kwa njia yao.

<sup>86</sup> Sasa huenda ikaja kwa njia iyo hiyo leo hii, tena, mnaona. Si ingekuwa vibaya sana kama ingekuwa hivyo? “Na sisi tumeichora yote, na tumekuwa na elimu nyingi mpaka tunaweka chati na kukuambia karibu saa ile Yeye anayokuja, na tunakuambia kama Yeye anaenda kupanda farasi mweupe ama wingu. Tunajua hakika jinsi inavyoenda kuwa.” Na huenda ikawa tofauti kabisa wakati Yeye ajapo. Naam. Alifanya. Mnajua, mambo hayo ni hatari sana ikifikia kujaribu kusema, “Hili ni *lile*.” Jinsi—jinsi tu Maandiko yameandikwa, hiyo ndiyo.

<sup>87</sup> Hivi mlitambua, wakati mmoja, nilitoa tamshi namna hii. Wakati mmoja wanafunzi walimwambia Yesu, katika... Ninaamini katika Mathayo Mtakatifu 6:11...ama 11:6, ninaamini ndiyo, samahani, 11:6, nafikiri ndiyo, ambapo wanafunzi wa Yohana walimjia Yesu na—na walitaka kujua ikiwa Yeye kweli alikuwa Ndiye. Sasa Yohana (alikuwa) amemtambulisha Yeye, na alikuwa yuko gerezani. Na sasa Yesu alisema, “Kaeni tu mpaka ibada iishe, halafu mrudi na mumwonyeshe Yohana kile mlichooni.” Sasa Yeye kamwe hakumpa kitabu juu ya jinsi ya kujiadhibisha gerezani, ama kitu kama hicho, ama hotuba fulani ya kiakili. Alisema, “Nyinyi kaeni tu karibu mpaka mkutano umalizike, ndipo mwende mumwonyeshe Yohana kile mlichooni.” Basi walipoenda, Yesu aliwatazama walipokuwa wakivuka kilima.

<sup>88</sup> Akasema, “Mlitoka kwenda kuona nini wakati mliopotoka kwenda kumwona Yohana? Je! mlienda kumwona mtu aliyevikwa nguo nzuri nyororo, na ukosi uliopinduliwa, na, mwajua, na kadhalika?” Kasema, “Hao ni wa ikulu za wafalme. Wanabusu watoto wachanga na kuzika wafu, na kadhalika.” Kasema, “Bali nyinyi mlitoka kwenda kuona nini? Mtu anayetikiswa na—na upepo, kama unyasi?”

<sup>89</sup> La, si Yohana. Huwezi kumwambia, “Nitakupatia kiasi fulani ukiacha kanisa hili na kuja huku kwenye *hili*.” Si Yohana. Yeye hakuyumbishwa huku na huku, na madhehebu na kadhalika. Si Yohana.

<sup>90</sup> Akasema, “Mlitoka kwenda kuona nini? Nabii?” Ndipo Yeye akasema, “Ninawaambieni, na zaidi ya nabii.” Lakini alikuwa zaidi ya nabii kwa sababu yeye alikuwa ndiye—ndiye... alikuwa ndiye ta—ta—ta—tao kati ya torati na neema. Alikuwa ndiye mjumbe wa agano la siku hiyo, mtu mashuhuri.

<sup>91</sup> Na tunakuta kwamba wakati Yeye alipokuwa akiongea, akizungumza kuhusu Yohana na kuhusu jinsi yeye alivyokuwa mtu mashuhuri, Yeye alisema, “Kama mnaweza kulipokea, huyu

ndiye yule ambaye nabii alizungumzia, ‘Nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.’” Unaona?

<sup>92</sup> Ndipo wao wakasema, “Vema, basi, kwa nini Eliya anasema...” Wakati mmoja Yeye alipokuwa akizungumzia hilo. Kasema, “Ni kwa nini Eliya alisema hivyo, kwamba kitu cha kwanza kilikuwa...” Ama, “Ni kwa nini waandishi wakasema,” samahani, “kwamba Eliya lazima aje kwanza?”

<sup>93</sup> Na Yeye akasema, “Eliya amekuja tayari na nyinyi hamkujua.” Unaona? Unaona? Watu hao waliofunzwa wakimtazamia huyo mtangulizi wa Yesu kuja, wamefunzwa katika kila njia ya Biblia, waandishi ambao waliandika Biblia na walijua Hiyo kuanzia A mpaka Z, nyuma, mbele. Watoa hotuba, jamani, walikuwa ni watu kwelikweli, walijua Maandiko ndani na nje, kila Neno, lakini hata hivyo walishindwa kuona kwamba Yohana alikuwa ndiye Eliya. Hata wanafunzi Wake hawakuliona.

<sup>94</sup> Sasa si ingekuwa vibaya sana, mojawapo ya siku hizi, kama tukiona hukumu ikiipiga dunia, na tuseme, “Vema, kwa nini hivi? Unyakuo unapaswa kuja.”

<sup>95</sup> Na Yeye angesema, “Mbona, umekuja tayari na nyinyi hamkujua.” Unaona? Unaona? Kwa dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, wakati hakuna mtu anayewazia hilo, nalo litanyakuliwa kisiri. Kamwe hutajua wakati likiondoka. Nakuambia, inatufaa sisi kuwa tayari, tuseme, na kuwa tayari kwa ajili ya wakati huu.

<sup>96</sup> Sasa hebu tuchukue na tuone kile Yeye alichokuwa. Tunaona, punde tu Yeye alipobatizwa, Mungu alikuja juu Yake, katika umbo la hua, ndipo Yeye akaenda nyikani kwa siku arobaini za majaribu. Na hapo Yeye alimshinda Shetani, juu ya Neno, kwanza. Alimshinda Shetani, juu ya Neno.

<sup>97</sup> Ndipo huduma Yake ya duniani ikaanza. Sasa tunamwona Yeye, kitu cha kwanza, kulikuwa na mtu jina lake Andrea, katika Yohana Mtakatifu 1. Tunaona kwamba alitoka akaenda na kumpata kaka yake, Simoni, na kumleta Simoni kwenye mkutano mahali Yesu alipokuwa akihubiri. Na wakati alipofanya hivyo, naye Yesu akamwona Simoni; upesi, wakati Yeye alipomwona, Yeye alimwambia jina lake lilikuwa “Simoni,” naye alikuwa ni “mwana wa Yona.” Sasa, basi, hilo liliondoa ugumu kutoka kwa mtume huyu, ndipo akamtambua Yeye basi kuwa ndiye Kristo; na hatimaye akawa kiongozi wa kanisa huko Yerusalemu, kwa sababu alikuwa ametambua kwamba Huyu alikuwa ni Kristo.

<sup>98</sup> Hivi uliwahi kuwazia kile kilichomfanya kumtambua Mtu huyu kuwa ndiye Kristo, kwa kusema tu hivyo? Kwa sababu kwamba Kristo, kulingana na Maandiko, alikuwa awe ni nabii. Musa, kiongozi wao na mwalimu, alikuwa amewaambia, “Bwana Mungu wenu atainua Nabii mithili Yangu.” Haijalishi

ni watu wangapi wenye elimu waliokuwa wameinuka, ilibidi aje Nabii, naye Nabii huyo ilibidi aonyeshe ishara ya nabii.

<sup>99</sup> Sasa labda ninazungumza na watu wengi Wayahudi, usiku wa leo. Na nyinyi mnajua, katika Maandiko, Myahudi alimwamini nabii wake. Kwa sababu, ilikuwa ni nabii ambaye Neno la Bwana lilimjia, yeye, na yeye pekee. Neno la Bwana liliwajia manabii. “Mungu, katika nyakati za kale na njia mbalimbali alinena na baba zetu kupitia manabii, bali katika siku hii ya mwisho kupitia Mwana Wake, Yesu Kristo,” Waebrania 1. Sasa, Myahudi alimwamini nabii kwa sababu nabii alikuwa na Neno la Bwana.

<sup>100</sup> Sasa, jinsi ambavyo walijua kama nabii huyo alikuwa sahihi au sivyo, ilikuwa kwa sababu walimtaazama nabii huyo. Na kama alisema chochote, akatabiri, na kikaja kutimia, Mungu alisema, “Msikieni nabii huyo, kwa kuwa niko pamoja naye. Lakini kisipokuja kutimia, basi puuzeni kile anachosema.” Hiyo si zaidi ya kweli, unaona. “Akiwepo mmoja, nabii miongoni mwenu, wa kiroho ama nabii, Mimi Bwana nitajitambulisha Mwenyewe kwake katika maono, kunena naye kupitia ndoto. Na iwapo kile nabii huyu anachosema kinakuja kutimia, basi msikieni, kwa kuwa niko pamoja naye. Lakini kisipotimia, basi msimsikie.”

<sup>101</sup> Kwa hiyo, Yesu akisimama pale. Na wao hawakuwa wamekuwa na nabii kwa miaka mia nne, katika Israeli. Basi hapa alisimama Mtu ambaye alimwona mvuvi wa kawaida akipanda juu, na kumwambia kile jina lake lilichokuwa na kile jina la baba yake lilichokuwa. Ni jambo la kushangaza jinsi gani! Yeye alikuwa anafanya nini? Alikuwa anamwita mtu huyo. Basi wakati Nuru hiyo ilipoangazia juu ya mbegu hiyo iliyokusudiwa kimbele, Uhai ukaja upeşi, alitambua kile ilichokuwa.

<sup>102</sup> Mtu huyu tunayemzungumzia sasa, Filipo, aliona hili likitendeka, kwa hiyo anakimbia kuzunguka mlima, ni yapata maili kumi na tano, na kuenda kwa rafiki ambaye alikuwa m—m—mchunguza Maandiko, pamoja na yeye. Naye, mtu huyu, jina lake lilikuwa Nathanaeli. Na hapana shaka alikuwa na kichaka, na kwa hiyo alikuwa huko nje kichakani, katika maombi, wakati Filipo alipowasili. Na wote wawili walikuwa Waebrania sasa, wakitazamia kuja kwa Masihi. Kwa hiyo wakati Filipo alipompata, alisema, “Njoo, mwone Yule niliyempata, Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu.”

<sup>103</sup> Na, bila shaka, Nathanaeli akiwa mtu mashuhuri, na akijua kwamba Nazareti ulikuwa m—mji mbaya, basi—basi alisema, “Laweza lolote jema kuja kutoka Nazareti?”

Akasema, “Njoo, uone.”

<sup>104</sup> Hilo ndilo—hilo ndilo moja ya matamshi yanayoshangaza mno! Watu wengi sana wata—wataketi mbali na kukosoa chochote, badala ya kuja na kukiweka moyoni, na kukichunguza na kuona kama ni sahihi. Kama wale waandishi wangefanya tu

hivyo kwa Yesu Kristo, ninii...nyinyi Wayahudi msingekuwa katika hali mliyomo sasa. Unaona? Na ulimwengu, makanisa yasingekuwa jinsi yalivyo sasa. Watu, tusingekuwa jinsi tulivyo, kama tulichunguza Maandiko na kama Mungu aliinua kitu. Tunajua kuna ushupavu mwingi; daima umekuwapo, daima utakuwapo, mpaka Yesu atakapokuja. Lakini basi, manabii wa uongo na makristo wa uongo, na kila kitu kingine, kinapaswa kuinuka ulimwenguni, kikionyesha nyakati za ishara, ishara za nyakati, hasa, na kadhalika. Lakini Yeye alisema, “Msiamini hayo.” Unaona? Bali sasa tazama, katika hili, hawakusimama kuwazia ni Nani, kitu gani kile Yeye alichokuwa akifanya.

<sup>105</sup> Filipo alisema, “Njoo, ujionee mwenyewe.” Kwa hiyo wakati Filipo na—na—na Nathanaeli walipotembea kando ya mlima, pamoja, wakaja mkutanoni karibu tu namna hii, tuseme, mahali Yesu alikuwa anazungumza.

<sup>106</sup> Sasa, sijui jinsi walivyokuja. Huenda alikuwa amesimama huko nje katika kusanyiko, yeye labda alishakuwa hapa juu mahali Yesu alikuwa, alikuwa anaombea wagonjwa. Ni ninii, hapana, hatuambiwi tu mahali pale walipokuwa. Bali punde tu Yesu alipomwona mtu huyo, Yeye alisema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!” Sasa tazama kile ambacho Yeye anajifanya Mwenyewe, ametambulishwa, wakati Yeye alipokuwa hapa jana.

<sup>107</sup> Unaona, Yeye kamwe hakutoa hotuba kubwa za kielimu. Hatuna kumbukumbu Yake kuelimishwa katika seminari, kama nilivyosema. Kamwe hakuandika kitabu. Hakuandika neno moja. Aliandika kitu fulani kwenye udongo, na kisha akachukua mkono Wake na kukifutulia mbali tena. Ni kwa nini Yeye hakuandika kitu? Kwa sababu Yeye alikuwa Neno.

<sup>108</sup> Kwa hiyo, unaona, kama wangejua tu, Yeye alikuwa ni Neno. Alikuwa ni Neno Lenyewe lililofanyika mwili. Alikuwa ni Mungu aliyefanyika mwili. Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.

<sup>109</sup> Sasa tazama kile Yeye alichofanya, wakati Filipo akimleta huyu Myahudi mwaminifu, Yeye alisema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake.”

<sup>110</sup> Vema, wengine huenda wakasema, “Hakika, wangeweza kujua, jinsi alivyokuwa amealia.” La, watu wote wa Mashariki walifunga vilemba, walikuwa na ndevu, walivaa mavazi. Usingeweza kumtofautisha na Mwashuru yeyote au mtu yeyote mwingine. Alivalia tu vazi la aina hiyo.

<sup>111</sup> Kasema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake.” Yeye alijuaje kwamba huyo alikuwa mtu huyo mwenye haki, mwaminifu ambaye alikuwa? Angeweza kuwa ha—haini. Angeweza kuwa mwizi ambaye alikuwa amekuja pale pamoja na Filipo. Hakuja, bali Yeye alikuwa na njia ya kujua.

<sup>112</sup> Na yeye, ilimshangaza mtu huyu sana, hata akasema, “Rabi,” ambalo linamaanisha *mwalimu*, “uliniona lini Wewe? Unanijua je Wewe?”

<sup>113</sup> Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya ule mti, nalikuona.” Unaona?

<sup>114</sup> Basi msomi huyu wa Neno alijua nini kwa hilo? Alijua huyo alikuwa ni yule Nabii. Akasema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.”

<sup>115</sup> Naye Yesu akasema, “Kwa sababu nilikuambia mambo haya, umeamini, sasa utaona makubwa kuliko hili.”

<sup>116</sup> Unaona jinsi Yeye alivyokuwa akijitambulisha Mwenyewe. Si katika vazi fulani, si katika ninii mashuhuri... kuwa mtoa hotuba mkubwa maarufu, shahada fulani ya udaktari kutoka chuo fulani.

<sup>117</sup> Mambo hayo ni sawa. Sikosoi. Ninajaribu kuvuta kutoa kitu fulani ambacho kinapaswa kutokea hapo, unaona, kuwaonyesheni. Hayo madhehebu na vyuo, na mavazi, kama ninavyojua, yote ni sawa, bali hatuzungumzi kuhusu mambo hayo sasa. Unaona? Kwa hakika afadhali nimwone mtu katika vazi la kidini kuliko kumwona kama baadhi ya hawa wanawake mtaani, unaona, au kitu fulani. Afadhali nimwone, hata kama yeye ni shupavu katika dini yake, afadhali nimwone namna hiyo kuliko kuwa hapa nje ameleva mahali fulani, katika shimo, unaona, kwa hiyo sina kitu cha kusema juu ya hilo.

<sup>118</sup> Bali kile ninachojaribu kusema, tunajaribu kumpata Mtu huyo, Yesu. Huyo ndiye Mtu tunayejaribu kumpata. Vipi kuhusu Neno hili? Hilo, je! Neno hilo linaweza kusema uongo? La, bwana, Hilo haliwezi kusema uwongo na liwe ni Mungu. Mungu hawezi kusema uwongo. Nalo Neno hili ni Mungu. Biblia ilisema Hilo lilikuwa. Basi kwa hiyo sasa tunajaribu kupata kile Yeye alichoko.

<sup>119</sup> Tungewezaje kumtambua Yeye? Si katika mavazi, si katika madhehebu, si katika hotuba. Tunaendaje kumpata Yeye? Tunaenda kumpata Yeye katika yule Mtu kile Yeye alichoko, alichoko Yeye sasa. Tazama, hivyo ndivyo walivyomjua Yeye huko nyuma. Si kwa mavazi Yake, si kwa elimu Yake kutoka shule Yake.

<sup>120</sup> Asingeweza kueleza shule yoyote ambayo Yeye alitoka. Kasema, “Umetoka wapi Wewe? Ni shule gani Yeye aliyotoka? Hatujui chochote kuhusu Mtu huyu.” Hakika, kamwe hawakuwa na kumbukumbu yoyote Yake mahali popote. Lakini Yeye...

<sup>121</sup> Hivyo ndivyo manabii walivyoinuka. Hawakujua mahali walipotokea. Hawajui chochote kuhusu Eliya, kuhusu hao wengine. Walikuja tu kutoka kusikojulikana, na kuondoka. Hayo ndiyo yote wajuayo. Ni watu ambao Mungu anaweza kuwashika. Watu kama wewe, ambao Mungu anaweza kuwashika na kujitangaza Mwenyewe, ili Yeye aweze kuhukumu

kizazi kwa njia ya haki, ili Yeye aweze kuhukumu taifa, kuhukumu ulimwengu. Kwa sababu, Neno halina budi kuenenda mahali fulani, na Yeye huhakikisha kwamba Wateule wanaingia ndani kusikia Hilo.

<sup>122</sup> Sasa tunaona, kwamba wakati Yesu alipokuwa—alipokuwa akizungumza, na Yeye anatambua, kulikuwa na wale... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

<sup>123</sup> Kulikuwa na wale ambao walisimama pale, ambao iliwabidi kujibu kwa kusanyiko lao. Kulikuwa na wale pale ambao iliwabidi kujibu kwa madhehebu yao, wawe Mafarisayo, Masadukayo, Waherodia, chochote wawezacho kuwa. Na kwa hiyo walisimama pale, ndipo wakasema, “Mtu huyu hufanya hayo kwa Beelzebuli. Yeye ni mpiga ramli,” kwa maneno mengine. “Yeye huwasiliana kimawazo. Yeye husoma akili yao.”

<sup>124</sup> “Yesu akitambua mawazo yao.” Haikuwalazimu kulisema kwa sauti. Alijua kile walichokuwa wanafikiria. Alishika mawazo yao.

<sup>125</sup> Ni yeye yule leo hii kama Yeye alivyokuwa wakati huo. Yeye anajua kile unachofikiria, unaona. Kama Yeye ni Neno, inabidi Yeye abaki kama Neno. Sasa, katika Waebrania 4, Biblia ilisema kwamba, “Neno la Mungu ni kali, lina nguvu kuliko, kali kuliko upanga ukatao kuwili, mtambuzi hata wa mawazo ya moyoni.” Ni kitu gani? Neno, Neno la Mungu linaweza kutambua mawazo yaliyoko moyoni mwako.

<sup>126</sup> Hilo hasa ndilo Yeye alilokuwa, Neno, nalo Neno liliweza kutambua mawazo yaliyoko moyoni. Unaona? Sasa, hilo ndilo Neno lilikuwa. Walipaswa kujua hilo, unaona, kwamba hiyo ndiyo sababu. Yeye aliyatambua mawazo yao, akawatazama. Ndipo Yeye akasema, “Nitawasamehe kwa ajili ya hilo,” kwa kuwa Yeye alikuwa hajasulubiwa bado. Roho Mtakatifu alikuwa hajaja.

<sup>127</sup> “Bali,” Yeye alisema, “atakapokuja Roho Mtakatifu,” kufanya jambo lile lile ambalo Yeye alikuwa anafanya, maana Yeye aliahidi Hilo lingefanyika, unaona, “wakati Roho Mtakatifu atakapokuja, Yeye atawakumbusha mambo haya, yale niliyowafundisha, na atawaonyesheni mambo yanayopaswa kuja.” Unaona? “Sasa wakati Yeye ajapo kufanya jambo lili hili ambalo ninafanya, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu na katika ulimwengu ujao.” Unaona, hivyo ndivyo itakavyokuwa kali katika siku hizi za mwisho. Unaona? Itatenganisha, unaona.

<sup>128</sup> Ndipo Mungu katika hukumu Yake, kama Yeye alivyofanya katika Edeni, Yeye anaweza kusema kwa haki, “Mliliona. Mnalijua. Nililithibitisha, na nyinyi hamkuliamini.” Jambo ndilo hilo.

<sup>129</sup> Sasa, pia tazama kile Yeye alichofanya wakati Yeye alipofanya hili, kile Yeye alichosema. Filipo alisema, “Wewe

ndiwe Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli.” Yesu alimwambia kwamba mambo makubwa kuliko haya yeye angesema. Sasa, hiyo ilikuwa kwa Wayahudi.

<sup>130</sup> Sasa zipo jamii tatu za watu duniani, kadiri ambavyo sisi—sisi tunataka kuamini, hizo ni: Myahudi, Mtaifa, na Msamaria. Sisi daima... Mungu anakamilika katika tatu. Na wapo wana watatu wa Nuhu, na kutokana na hao wana watatu walileta jamii yote ya watu.

<sup>131</sup> Tunaona sasa, kwamba, Roho Mtakatifu. Petro kwenye siku ya... kabla ya Siku ya Pentekoste, alipewa funguo za Ufalme. Tunaona kwamba alifungua Huo kwa Wayahudi, kwenye Siku ya Pentekoste. Ndipo akaenda huko chini Samaria, na kufungua Huo kwao. Akarudi kwenye nyumba ya Kornelio, na kuufungua Huo hapo. Na kamwe haikumbidi kufanya hivyo tena; Huo ulikuwa umefunguliwa kwa ulimwengu, unaona, namna hiyo, Roho Mtakatifu. Lakini unakumbuka, Filipo alienda huko chini na kuwahubiria Wasamaria, na alikuwa amewabatiza katika Jina la Bwana Yesu, ila tu Roho Mtakatifu alikuwa hajashuka juu ya yeyote wao bado; kwa hiyo walituma mtu kwake yeye aliyekuwa na funguo, ndipo yeye akaweka mkono wake juu yao, na Roho Mtakatifu akaja juu yao. Hiyo ni kweli. Hao ni Wayahudi, Mat-... hizo jamii tatu za watu.

<sup>132</sup> Sasa, sisi Mataifa, tulikuwa makafiri, Warumi, Wayunani, na kadhalika. Tuliabudu sanamu. Hatukuwa tukimtaambia masihi yeyote. Hatukuwa na wakati kwa ajili ya Masihi yeyote. Tulikuwa na miungu yetu wenyewe, babu zetu. Bali Wayahudi walikuwa wakitazamia Masihi. Na vivyo hivyo na Wasamaria, kwa sababu walikuwa nusu Myahudi na Mtaifa.

<sup>133</sup> Sasa, Yesu ataonekana kwa wale ambao wanamtazamia Yeye; hao pekee, hivyo tu. Yeye hawajibiki kwa asiyeamini. Bali kwa mwaminio Yeye anawajibika. Anawajibika kumfufua mwaminio, unaona, katika siku ya mwisho, kwa mwaminio pekee.

<sup>134</sup> Sasa tunaona, kwamba Yesu hapa alikuwa amejitambulisha Mwenyewe kwa Myahudi. Ambao, tuna wengine wengi, tungeweza kumchukua Bartimayo kipofu, bali ili kuokoa wakati... Walikuwa wengine wengi kupitia Maandiko, hasa akiwathibitishia kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, kwa kuwa Nabii. “Bwana Mungu wenu atawainulia Nabii mithili Yangu.”

<sup>135</sup> Hawakuwa wamekuwa na manabii. Lakini wale ambao walikuwa wameondokea wazo kwamba Yeye alikuwa Nabii, iliwabidi kutoa jibu kwao, kwa hiyo walisema tu, “Yeye alikuwa pe—pepo, mchawi, ama, mnajua, roho fulani mwovu akifanya hayo.”

<sup>136</sup> Na Yeye alisema kwamba, “Tlikuwa ni dhambi isiyosameheka, kuita kazi ya Roho Mtakatifu, ‘roho mwovu,

kitu kiovu,' kwamba, Roho Mtakatifu akija na kudhihirisha Neno Lake."

<sup>137</sup> Kwa nini? Ilikuwa imetabiriwa kwamba Yesu angefanya jambo lili hili. Wakati Yeye alipowaambia Wayahudi, Yeye alisema, "Vema, ni yupi kati yenu awezaye kunihukumu Mimi? Ni yupi kati yenu awezaye kunishtaki Mimi kuwa nina dhambi?" *Dhambi* ni "kutokuamini." Kama... Yeye alisema, "Yachunguzeni Maandiko, maana ndani yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Walipaswa kujua hilo. Walidhania kuwa walijua hilo; lakini, hawakujua, wangelijua Yeye alikuwa ni Neno pale pale. Yeye aliweza kutambua mawazo hasa katika mioyo yao, na kadhalika, na kufanya hasa kabisa kile manabii walichofanya.

<sup>138</sup> Kwa sababu, Yeye alikuwa zaidi ya nabii, Yeye alikuwa ni Mungu wa manabii. Alikuwa ndiye kichwa na wa—wa mwisho kati ya manabii. Leo hii Yeye anazungumza, Mwenyewe, kupitia Kanisa Lake.

<sup>139</sup> Sasa tukitambua hapa ndani, kwamba, Yeye alijitambulisha Mwenyewe kikamilifu na Wayahudi, kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, kwa kuthibitisha Yeye alikuwa ni Nabii. Tunajua hilo. Hakuna njia nyingine. Si kwa vazi Lake, si kwa kuongea Kwake, si kwa chochote kingine bali kwa kuwa...

Na halafu unasema, "Vema, Yeye alitoa pepo."

<sup>140</sup> Alidai kwamba Mafarisayo walifanya jambo lile lile. Akasema, "Kama nikitoa pepo, kwa kidole cha Mungu, watoto wenu wanazitoa kwa kitu gani?" Unaona? Kwa hiyo walikuwa wakitoa pepo, pia. Unaona? Kwa hiyo, lakini Yeye alikuwa akizitoa kwa kidole cha Mungu, kasema, "Basi Ufalme wa Mungu umekuja karibu nanyi."

<sup>141</sup> Sasa tunaona kwamba kitu ambacho kilimtambulisha Yeye hasa kuwa Ma—Masihi, kilikuwa ni nabii, kwa sababu *Masihi* maana yake "Yule aliyetiwa upako." Na kutiwa upako na kitu gani? Neno. Neno lililotiwa upako ni kama tu mbegu iliyo na maji juu Yake, katika udongo mzuri, Hiyo huzaa hasa ahadi Yake. Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, "Ni nani awezaye, ni nani awezaye kunihukumu Mimi? Ni nani anayeweza kuniambia Mimi kwamba mimi... Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Na hili ndilo Neno. Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Kama sitendi kile Neno hili liliahidi kwa ajili ya kizazi hiki, basi msiniamini Mimi," Yeye alisema.

<sup>142</sup> Loo, si ingekuwa ajabu, leo hii, kama kanisa lingeweza kusema jambo lilo hilo, tungsimama hapo? Hili, kama hatuzitendi kazi za Mungu, basi si Mungu. Na kila mahali alipo Mungu, mambo ya kimbinguni hutukia, kwa sababu Yeye ni wa kimbinguni. Unaona, Yeye ni—Yeye ni Roho. Mungu ni Roho.

<sup>143</sup> Sasa tunakuta kwamba Yeye anaenda huko chini Yeriko, bali Yeye alikuwa na haja kupitia Samaria. Sasa, Samaria ni nyuma ya mlima. Yeriko uko chini sehemu ya chini ya kilima. Lakini njiani Mwake akiteremka, badala ya kuenda moja kwa moja huko chini Yeriko, Yeye anazunguka kupitia Samaria. Najiuliza ni kwa nini? Ndipo Yeye akafikia mji uitwao Sikari. Na wao... akatuma wanafunzi mjini kununua maakuli, chakula.

<sup>144</sup> Basi wakati walipokuwa mjini kununua chakula, Yeye aliketi chini kando ya kisima. Na kilikuwa ni kisima, kama mandhari kidogo, kama, katika mahali pa mkutano wa umma kwa ajili ya watu kuja kuteka maji yao. Na kingalipo leo hii. Na mizabibu ilikuwa imeota juu ya ukuta, naye Yesu alikuwa ameketi kuegemea ukuta.

<sup>145</sup> Basi wakati Yeye alipoketi hapo, kulikuwa na msichana aliyekuja kutoka mjini. Tungetaka kumwita, leo hii, mwanamke mwenye sifa mbaya. Na labda mtoto huyo alisukumwa kuingia kwenye hiyo, na, yeye, labda wazazi wake walimwachilia kwenda mtaani. Na mnajua ninachomaanisha. Pia nafikiri msichana huyo, mwanamke, hasa jambo fulani lilikuwa limetendeka; hatujaambiwa katika Maandiko, bali tazama kile kilichofanyika kwa moyo wa mwanamke huyo. Unaona? Alikuwa kuteka maji, na hapana shaka ilikuwa yapata adhuhuri.

<sup>146</sup> Kwa kawaida wanawali, hata wa leo, hutoka mapema asubuhi na kuteka maji yao, na kuyatweka vichwani mwao, katika vyombo vyao vikubwa vya udongo, na wanayabeba kufanya maji yao ya kunywa na kazi yao ya nyumbani, na chochote wanachoenda kufanya.

<sup>147</sup> Basi msichana huyu alitokea yapata adhuhuri. Kwa nini? Yeye asingeweza kuhusishwa na watu wengine, wa—watu wazuri. Asingeweza kushikwa miongoni mwao. Wangemkwepa, na yeye alijisikia vibaya kuhusu hilo, kwa hiyo yeye angekaa nyuma. Alijua aina ya maisha ambayo alikuwa anaishi, kwa hiyo alikaa mbali na watu wa kidini.

<sup>148</sup> Sasa tunaona, alipotoka nje, yeye labda hakumtambua Yule aliyekuwa ameketi pale ameegemea ukuta.

<sup>149</sup> Na hiyo mitungi waliyo nayo, ambayo ninaiita. Hiyo ni... Baadhi yao huiita ndoo. Ina mikono. Imetengenezwa na—na udongo. Pia wana winchi, na kulabu mbili tu zinazolingia ndani. Wanaishusha chini ndani ya kisima. Na kwa kuwa... kuipindua nayo inajaa maji, na kuivuta juu tena kwa winchi. Nao wanaibeba juu ya vichwa vyao, na juu ya nyonga zao, wanapotembea.

<sup>150</sup> Naye mwanamke huyu labda alikuwa karibu tu kuweka kulabu juu ya m—mtungi, na alikuwa tu karibu kuishusha chini, ndipo akasikia Sauti, kasema, “Mwanamke, niletee maji ninywe.” Ndipo mwanamke akaangalia kuona Huyo alikuwa ni nani. Na hapo aliketi labda, takriban, kama Myahudi mwenye

umri wa makamo ameketi hapo. Na Yeye hakuwa ila yapata umri wa miaka thelathini na kitu, umri wa miaka thelathini na miwili au thelathini na mitatu, wakati huo.

<sup>151</sup> Na, bali hapana budi Yeye alionekana mwenye umri mkubwa zaidi kidogo kuliko kile Yeye alichokuwa, kwa sababu Yeye alikuwa ameitwa, Yohana Mtakatifu 6, kuwa wa miaka hamsini. Kasema, “Wewe ni mtu si zaidi ya umri wa miaka hamsini, na Wewe unasema Wewe umemwona Ibrahimu? Sasa tunajua Wewe una kichaa. Wewe ni mwendawazimu,” ambalo linamaanisha *kichaa*. “Una pepo.”

Akasema, “Kabla Ibrahimu hajakuweko, MIMI NIKO.” Unaona?

<sup>152</sup> Sasa, Yeye lazima aliingia mvi kidogo, au kitu fulani. Alikuwa ameketi hapo, kwa namna fulani mwanaume aliyeonekana mwenye umri wa makamo. Ndipo Yeye... Mwanamke akasema, “Mbona, si kawaida.” Unaona, kulikuwa na u—ubaguzi miongoni mwao. Hawakuwa na uhusiano kati yao. Kasema, “Si kawaida kwenu Wayahudi kuomba Wasamaria fadhili namna hiyo.”

Akasema, “Lakini kama ulijua ni Nani uliyekuwa unazungumza naye!”

<sup>153</sup> Unaona, loo, hilo hapo! Kama tungalijua tu, loo, tunaposoma hili, ni Nani tunazungumza naye, unaona. Wakati unapoomba, ikiwa wewe... Yesu alisema, “Unapoomba, amini kwamba unapokea kile unachoomba.” Unaona?

<sup>154</sup> “Kama ungaliujua tu ni Nani uliyekuwa ukizungumza naye, ungeniomba Mimi maji, nami ninge kuletea maji ambayo huypati kutoka kwenye kisima hiki.”

<sup>155</sup> Ndipo ma—mazungumzo yakaendelea kidogo. Mwanamke akasema, “Vema, baba yetu...” Unaona, yeye akiwa Msamaria, hata hivyo alisema, “Baba yetu, Yakobo, alichimba kisima hiki. Na yeye alikinywea, na watoto wake, na kunywesha ng’ombe, na kadhalika.” Bali Yeye akasema... “Mbona, nyinyi mnasema, ‘abudu katika Yerusalemu,’ na—na wengine, ‘abudu katika mlima huu,’ na kadhalika.”

<sup>156</sup> Akasema, “Sisi... Wayahudi, wokovu ni wa Wayahudi. Tunajua kile tunachoabudu. Bali,” kasema, “nisikie Mimi. Wakati unakuja, na ni sasa, ambapo Baba anawatafuta waabuduo wa kweli, watakuwa wakiabudu katika Kweli na katika Roho.” Unaona, Roho na katika Kweli!

<sup>157</sup> Ndipo mazungumzo yao yakaendelea kwa ki—kitambo kidogo. Yeye alikuwa anafanya nini? Sasa karibu itawabidi kuchukua neno langu kwa ajili ya hili. Unaona, nafikiri Yeye alikuwa anajaribu kupata mahali shida yake ilipokuwa, kilichokuwa niani mwake. Sasa, kumbukeni, Baba alikuwa

amemtuma huko juu, “Nina haja kupitia Samaria.” Sasa Yeye alisema . . . Na hiyo ni Yohana Mtakatifu 4.

<sup>158</sup> Sasa katika Yohana Mtakatifu 5:19, wakati Yeye alipokuwa amemponya mtu yule kwenye lango liitwalo Zuri, tunajua Yeye . . . La, samahani, Yeye alikuwa kwenye birika la Bethesda. Alimponya mtu huyu, na aliulizwa ni kwa nini Yeye hakuwaponya wale wengine.

<sup>159</sup> Sasa, mtu huyo. Kulikuwa na watu waliokuwa wamelala hapo ambao walikuwa vilema, viwete, waliopooza, vipofu. Ndipo hapa Yeye akaja akitembea kupitia hapo, akitembea kupitia birika hili, na Yeye akamwendea mtu fulani, ambaye, sijui alikuwa na nini. Huenda alikuwa na TB, shida ya tezi dume, kitu fulani. Alikuwa amedumaa, alikuwa amekuwa nayo kwa miaka thelathini na minane, haikuwa inaenda kumwua. A—angeweza—angeweza kutembea, angeteremka chini.

<sup>160</sup> Lakini tazama, Yeye alikuja moja kwa moja kupitia umati huo wa watu, ambapo wote walikuwa hapo, umati, maelfu ya hao, walipokuwa wameketi kwenye lango la kondoo, “wakingojea kutibuliwa kwa maji.” Mungu daima amekuwa na njia kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu, kwa ajili ya watu. Basi kwa hiyo yule anayetangulia kuingia angekuwa na imani ya kutosha, ilichukua nguvu kutoka kwenye maji, aliponywa.

<sup>161</sup> Lakini tazama, Mtu huyu Yesu alikuja kupitia pale, ambaye alikuwa ndiye Mungu hasa wa uumbaji, na Yeye alikuja kupitia lango, na kuchanganyika miongoni mwa watu, wazia tu, akiwa na huruma. Je! mnaamini Yeye alikuwa na huruma? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

<sup>162</sup> Sasa simama tu kwa dakika moja na uwazie hili. Yupo mama aliye na mtoto mchanga mwenye kichwa kilichojawa maji labda ukubwa *huu* kote, amepitia moja kwa moja. Na hapa alikuwapo mwanamume ambaye alikuwa kipofu, “Mtu anirehemu na kuniweka ndani ya birika.” Biblia ilisema walikuwa walemavu, vipofu, viwete, waliopooza. Maskini mwanaume fulani amelala hapo, ambaye labda mikono yake haikuwa mikubwa *hivyo* kuzunguka. Ama, maskini mama mwenye lundo la watoto nyumbani, naye Yesu mwenye huruma alipita moja kwa moja karibu naye. Hilo ni ajabu? Na, hata hivyo, amejaa huruma. Lakini hiyo ni Biblia. Mtu yeyote . . . Unaona, sasa tazama. Hatujui kile huruma inachomaanisha.

<sup>163</sup> Mwangalie Yeye. Alimkuta mtu amelala juu ya godoro la majani makavu, ambaye aliweza kutembea, na Yeye akamwambia, “Wataka kuwa mzima?” Kwa nini huyo mmoja? Unaona, kwa nini huyo? Sasa angalia na Yeye atakuambia. Yesu alijua mtu huyu alikuwa amekuwa hapo katika wakati huu, unaona, miaka hii yote. Alimponya, akamwambia achukue kitanda chake na kuenda nyumbani. Na alifanya hivyo.

Walimpata akibeba kitanda chake, na kumpata Yesu na kumleta Yeye mbele za mahakama.

<sup>164</sup> Sikiza kile alichosema. “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda lolote Mwenyewe, bali kile ambacho Yeye amwona Baba analitenda.” Hiyo hapo huruma, kujua mapenzi ya Mungu na kisha kuyatekeleza. Unaona? Unaona? “Mwana hawezi kutenda lolote Mwenyewe, ila lile ambalo Yeye anaona,” si analosikia. Si... Unaona? “Lile ambalo Yeye amwona Baba analitenda, hilo atenda Mwana vile vile.”

<sup>165</sup> Kwa hiyo hapana shaka alikuwa na o—ono la kuenda huko juu, “Alikuwa na haja kupitia Samaria,” na Yeye alijua mwanamke huyu angekuwa hapo. Kwa hiyo akijua hilo, Yeye alikuja tu hapo juu na kuwa kwenye lango hili, akawatuma wanafunzi mbali. Ninii... Ndipo Yeye hakujua la kufanya wakati mwanamke huyo alipoanza kuuliza maswali haya, na kadhalika, kwa hiyo Yeye alimngojea tu Baba kumwonyesha Yeye. Ndipo wakati Yeye alipogundua kile shida yake ilichokuwa... Ni wangapi wanajua kile ilichokuwa? Mwanamke huyo alikuwa na waume wengi kupita kiasi. Na kwa hiyo Yeye alimwambia, kasema, “Nenda kamwite mume wako na mje hapa.”

<sup>166</sup> “Mbona,” mwanamke huyo akasema, “Sina mume.” Hilo lilionekana kuwa kemeo la moja kwa moja. Unaona?

<sup>167</sup> “Mbona,” Yeye alisema, “umesema kweli, kwa sababu umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa si mume wako. Katika hilo sasa wewe umesema kweli, ‘huna mume.’”

<sup>168</sup> Mwangalie maskini mwanamke huyo. Unajua, angeweza kufundisha asilimia tisini ya makasisi, leo hii, Injili. Unaona? Mbona, mbona wale makuhani walisimama pale na kumwita Yeye “Beelzebuli,” wakati Biblia yao yenyewe ilisema hilo ndilo Yeye angefanya? Je! hiyo ni kweli? Na hapa anasimama kahaba, mwanamke mwenye sifa mbaya, tena, punde tu Yeye alisema hilo kwa mwanamke huyo, kamwe hakusema, “Vema, Wewe ni Beelzebuli.”

<sup>169</sup> Mwanamke huyo alisema, “Bwana, ninatambua kuwa Wewe ni nabii.” Sasa tazama nukuu yake. “Tunatambua, ninatambua kwamba Wewe ni nabii. Tunajua kwamba wakati Masihi ajapo, ambaye anaitwa Kristo; tunamtazamia Yeye kuja, na, wakati Yeye akija, Yeye anaenda kutuambia mambo haya. Hili ndilo Yeye anaenda kufanya.”

<sup>170</sup> Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi, jana. Hiyo ndiyo ishara ya Masihi, leo, ile ile. Unaona?

<sup>171</sup> “Tunajua wakati atakapokuja Masihi, Yeye atatuambia mambo haya, lakini Wewe ni Nani?” Hilo lilikuwa ndilo swali. “Ninajua Wewe ni nabii. Hatujakuwa na mmoja kwa mamia na mamia na mamia ya miaka.”

“Nyaraka za mababu wa mababu wa mababu wa mababu wa baba zetu hapa zilisema walikuwa na nabii, yule wa mwisho, Malaki, miaka mia nne na kitu iliyopita; hatujakuwa na nabii kamwe katika Israeli tangu, bali hapa amesimama Mtu akiniambia hili.”

“Wewe ni nabii. Na sisi tunatazamia Masihi.”

Yesu alisema, “Mimi Ndiye, ninayezungumza nawe.”

<sup>172</sup> Huo ndio utambulisho Wake. Hivyo ndivyo Yeye alivyojitambulisha Mwenyewe kwa Israeli. Yeye Huyu hapa na Wasamaria, akijitambulisha Mwenyewe.

<sup>173</sup> “Mimi Ndiye, ninayezungumza nawe.” Na, juu ya hayo, hakuliswali hilo. Unaona, Uhai ulijulikana kimbele na Mungu.

<sup>174</sup> Basi haijalishi ni kiasi gani hao Mafarisayo walivyojaribu kuwa wa kidini, Yesu alisema, “Wao, wao walikuwa wamepofushwa.” Akasema, “Isaya alinena vema juu yenu, ‘Mnayo macho, na hamwezi kuona. Mnayo maarifa, na hamwelewi.’ Wewe ni mhadhiri, na hujui kile unachozungumzia. Nyinyi ni, mnaona, mnayo mambo haya yote.”

<sup>175</sup> Kwa sababu, unaona, Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu isipokuwa Baba Yangu amvute, na wote ambao Baba amenipa Mimi watakuja Kwangu.” Na Yeye alisema hivyo, siyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Unaona?

<sup>176</sup> Ilikuwa ni kitu gani? Kulikuwa na Biblia, ilisema, katika Waeb-...katika Kitabu cha Ufunuo. Katika siku za mwisho wakati “mpinga Kristo” alipoinuka ju—jukwaani, karibu sana kama kitu halisi, “ingedanganya mteule mwenyewe kama yamkini.” Bali, na ndipo Yeye akasema tena, “aliwadanganya wote juu ya uso wa dunia, ambao majina yao hayakuandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo, aliyechinjwa kabla ya msingi wa ulimwengu.”

<sup>177</sup> Unaona, majina yao yaliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima, Kitabu cha Ukombozi. Yesu alikuja kukomboa wale ambao majina yao yalikuwa ndani ya Kitabu. Na wakati jina hilo la mwisho limekombolewa, Mwana-kondoo anachukua Kitabu na kuondoka; hayo ndiyo yote, ukombozi umekamilika, umefungwa. Hao!

<sup>178</sup> Na huyo mwanamke alikuwa ni kitu gani? Alikuwa ni mmoja ambaye jina lake lilikuwa Huko. Haijalishi namna ya hali ile aliyokuwemo pale, punde tu Nuru hiyo ya Injili ya kweli ilipommulika maskini huyo kahaba, yeye aliitambua Hiyo. Kwa nini? Kulikuwa na kitu ndani hapo cha kuiwasha moto. Unaona, yeye aliitambua Hiyo.

<sup>179</sup> Huenda ukamimina maji kwenye petroli, hayo yataizuia tu; bali hebu moto kidogo uigonge wakati mmoja, na uangalie kinachotendeka, unaona. Inahitaji kuwashwa moto na imani,

kwa Neno la Mungu. Wakati wanapojua ni Kweli, kuna jambo fulani linatukia!

<sup>180</sup> Mwanamke huyo kamwe hakuuliza swali moja zaidi. Alijua huyo alikuwa ni yule Masihi. Kwa nini? Alikuwa amejitambulisha Mwenyewe kikamilifu. Kama tu vile Filipo alivyosema, “Mbona, Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli!”

<sup>181</sup> Kulikuwa na wale pale, kasema, “Huyo ni, Yeye ni mpiga ramli, hicho ndicho Yeye alichio.”

<sup>182</sup> Akasema, “Huwezi kusamehewa hilo, wakati Roho Mtakatifu akifanya hilo.” Unaona? Akasema.

<sup>183</sup> Lakini sasa tazama hapa jinsi Yeye alivyotambulishwa kwa mwanamke huyo. Ndipo mwanamke akakimbia upesi akaingia mjini, na yeye akawaambia wanaume.

<sup>184</sup> Sasa, kwa kweli, kama kuna yeyote wa Mashariki hapa, wewe, Biblia ni kitabu kipya kwa—kwa mtu kutoka Magharibi, anayeenda Mashariki mara moja, unaona, kwa sababu desturi zote, wangali wanaziishi vile vile. Mwanamke huyo hakuwa na haki kuingia mjini na kuzungumza na wanaume. Asingeweza kufanya hivyo. Kwa kweli wasingemsikiliza mwanamke huyo.

<sup>185</sup> Lakini alikuwa na ujumbe, ambao hakuna kitu kingeweza kumkomesha. Unaona, alikuwa amepata Uzima, kitu fulani kilichogonga. Aliingia mjini mbio na kuwaambia wanaume, “Njoni, mwone Mtu ambaye aliniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyo kuwa ndiye Masihi? Hicho si ndicho kile ambacho tumekuwa tukitazamia?”

<sup>186</sup> Alitambulishwa kama Masihi! Nayo Biblia ilisema kwamba, wakati Yesu alipoingia mjini, Yeye kamwe hakufanya hilo mara nyingine zaidi, si kwa hao. Bali waliamini kile mwanamke yule alichosema, unaona, na wao walimpokea Yeye. Yeye kamwe hakumponya mgonjwa yeyote; Yeye alijua Filipo alikuwa anashuka chini kufanya hilo, kwa hiyo, na kuwanyosha, baada ya Roho Mtakatifu kuja, kwa hiyo Yeye aliwafanya tu wajue kwamba Yeye alikuwa ni Masihi.

<sup>187</sup> Sasa tazama, kulikuwa na Wayahudi, walimtambua Yesu. Yeye alitambulishwa katika mwisho wa majira yao, kama Masihi, na hivyo ndivyo Yeye alivyofanya hilo.

<sup>188</sup> Vivyo hivyo na Wasamaria, walikuwa wakimtazamia Masihi. Hivyo ndivyo Yeye alivyojitambulisha Mwenyewe kama Masihi.

<sup>189</sup> Sasa imekuwa miaka elfu mbili na Mataifa, walipokea Injili. Sasa majira yetu yanamalizika, wakati wa kanisa, tunamalizia. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kamwe habadilishi mipango Yake. Basi ikiwa Yeye alisimama miongoni mwetu, usiku wa leo, Yeye asingekuwa ni mwanaume aliyevalia mavazi makubwa ya kikasisi, mzungumzaji stadi wa hotuba, au mhadhiri, au kitu fulani, bali Yeye angethibisha kwetu

kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Unaona? Alisema, wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa kwenye Kuja kwa Mwana wa Adamu.”

<sup>190</sup> Tazameni hili kwa makini sana. Katika siku za Sodoma, na daima, kumekuwa na matabaka matatu ya watu.

<sup>191</sup> *Tatu* ni idadi “kamilifu,” tunajua. Na *saba* ni “ukamilishaji.” *Arobaini* ni “kujaribiwa.” *Hamsini* ni “yubile.” Mnajua hisabati ya Maandiko.

<sup>192</sup> Lakini sasa tazama, huko—huko Sodoma, kulikuweko matabaka yako matatu ya watu. Kulikuwa na Wasodoma wako, ambao walikuwa ni wasioamini. Kulikuweko Lutu na kundi lake, ambao walikuwa ni waaminio vuguvugu, kanisa la kimwili. Kulikuwa na Ibrahimu, wa kiroho, aliyeitwa akatoka, mteule, nje huko nyikani mbali na Sodoma.

<sup>193</sup> Tazama, Malaika watatu walishuka toka Mbinguni, siku moja. Dhambi za Sodoma zilikuwa karibu mbaya kama ilivyo ulimwenguni leo. Walishuka chini. Sasa, Wao walionekana kama wanadamu, Wao walivalia nguo kama wanadamu wanavyovaa; vumbi juu Yao, na miguu Yao ilikuwa imechafuka kutokana na kutembea. Ndipo Ibrahimu, akiwa ameketi chini ya mwaloni, akawaona Wao wakija kwa mbali.

<sup>194</sup> Sasa tunarejea kwenye kile Yesu alichosema kufanyika kwenye wakati wa mwisho, kabla tu ya Kuja Kwake. Sasa, kumbukeni, Wasodoma walikuwa Mataifa.

<sup>195</sup> Tazama sasa, tunaona kwamba, hapa Wao walikuja, Watu hawa. Naye Ibrahimu, kiroho, alitambua kwamba kulikuwa na kitu fulani kuhusu Watu hawa tofauti na wageni wa kawaida.

<sup>196</sup> Kuna jambo fulani tu, wakati mwaminio anapokutana na mwaminio, wakati mwaminio anapokutana na Neno! Wakati, kitu kama yule mwanamke, unaona, wao—wao wamekusudiwa Hilo. Hawawezi tu kujizuia kuamini Hilo. Kuna kitu kinawagonga, unaona, wanalo Hilo.

<sup>197</sup> Basi wakati Ibrahimu alipowaona Watu hawa wakija, alitoka nje. Ndipo akasema, “Bwana wangu, je! unaweza kukaribia na kuniruhusu nichote maji kidogo nikaoshe miguu Yako? Na mimi nitakupa kipande cha mkate, mkononi Mwako, ndipo uende Zako, kwa kuwa huo ndio uliokuleta Wewe.” Wakageuka.

<sup>198</sup> Sasa, katika hema kubwa la bwana, ndipo alipoishi Ibrahimu. Nao wengi wa watumishi wake, wa kutosha kupigana na jeshi, waliishi nje kote hapo. Walikuwa wachunga mifugo. Kwa hiyo akakimbia na kumwambia Sara, mke wake, “Nenda ukande unga, au posho.” Mnajua, ukande, uuchunge, kwa namna fulani. “Na utengeneze keki kadhaa na uweke juu ya meko.” Na—na kisha, pia, alitoka nje akaingia kwenye kundi la mifugo na kupata ndama aliyenona, na—na kumchinja, na

kumkabidhi mtumishi fulani, na kusema, “Mchune ngozi, na utengeneze mno—mnofu fulani.” Na akaenda nje na kuzungumza na Watu hao.

<sup>199</sup> Upesi, alienda huko nyuma na kuchukua unga na m—mkate, na kuchukua maziwa na nyama, akatoka na kuiweka chini mbele Zao. Na Biblia ilisema, “Walikula. Walikula.”

<sup>200</sup> Na wewe unatambua, yule Mtu mmoja alishikilia kutazama kuelekea Sodoma. Ndipo Yeye akasema, “Sitaiweka hii kuwa siri.”

Wawili wa Hao wanasimama na kuendelea. Wanashuka kuenda katika Sodoma.

<sup>201</sup> Billy Graham mamboleo na Oral Roberts, na kwa hiyo Wao wako njiani Mwao wakiteremka, unaona, wanaenda chini kuingia kwa Wasodoma, kulipua Injili kama Billy Graham na hao wanavyofanya. Je! mliwahi kutambua? Wekeni hili sasa. Ninatumaini sisemi chochote kibaya. Bali, tumekuwa na hili, kiroho.

<sup>202</sup> Lazima—lazima usiangalie mambo kwa njia ya kimwili. Angalia roho ya kitu chochote. Unataka kuangalia jiji, angalia roho yake. Unaangalia familia, angalia roho zilizoko katika familia. Unamwangalia mwanaume, angalia roho iliyoko ndani yake. Unaona, chochote unachoangalia, kila kitu hakina budi kuwa na lengo na madhumuni. Unaona?

<sup>203</sup> Basi tazama hapa, hivi ulijua, watu wote mashuhuri ambao tumekuwa nao, Sankey, Finney, Moody—Moody, Knox, Calvin, na kadhalika, hakujawahi kuwa na mtu bado, hudumani, akiwa na huduma kwa kanisa baridi, ambaye aliishia na h-a-m, kama A-b-r-a-h-a-m, G-r-a-h-a-m. Kamwe hapo kabla. Yeye yuko moja kwa moja miongoni mwa Sodoma, hiyo ndiye sababu. Mtu huyo anafanya kazi ya ajabu. Hapo ndipo yeye anapaswa kuwa, unaona, *h-a-m* maana yake “baba wa mataifa.” Unaona?

<sup>204</sup> Angalia sasa, mmoja wao alienda huko chini kuwahubiria Wasodoma. Walienda huko chini.

<sup>205</sup> Mmoja wao alibaki hapa na Ibrahimu. Angalia sasa, alikuwa ni “Abramu” siku chache kabla ya hapo. Na mke alikuwa “Sarai,” si S-a-r-a-h. Unaona? Ni r-a... Na yeye alishakuwa ni A-b-r-a-h-a-m sasa. Basi, tazama, Yeye alimwita kwa jina lake jipya, “Abraham, yu wapi mke wako, S-a-r-a-h, Sarah? Yuko wapi?”

<sup>206</sup> Wanawake wakati huo walikuwa tofauti kidogo na walivyo sasa, unaona, hawakutoka nje katika shughuli za waume wao. Walikuwa nyuma, kukaa... Yeye alikuwa nyuma katika hema. Kwa hiyo yeye akasema, alisema, “Yuko katika hema, nyuma Yako.”

<sup>207</sup> Yeye akasema, “Ibrahimu, Mimi,” kiwakilishi nafsi, “ninaenda kukuzuru kulingana na ahadi ambayo nilikufanyia.”

Huyo alikuwa ni nani? Unaona? Alikuwa ni nani Mtu huyu aliyeketi pale amevaa nguo zenye vumbi? “Nitakuzuru kulingana na ahadi ambayo nilikufanyia.”

<sup>208</sup> Ndipo Sara, akiwa ni mwanamke mkongwe, yeye kwa namna fulani, kama ambavyo tungeliita leo hii, kwa namna fulani alibeza, mwajua, alicheka kifichifichi. “Mimi, mwanamke mkongwe?” Alikuwa na umri wa miaka mia moja sasa, unaona. Kasema, “Mimi, mwanamke mkongwe, mkongwe; na bwana wangu,” ambaye alikuwa ni mume wake, “akiwa mkongwe, pia, tuwe na raha?” Sasa sisi ni kusanyiko lililochanganyikana, bali mimi. . . Wewe humsikiliza daktari wako; na mimi ni ndugu yako. Unaona, kwa hakika kama—kama—kama tendo la kijamii, lilikoma, miaka mingi, mingi, unaona, na kwa hiyo wao—wao hawakuwa na uhusiano wa kifamilia. Ndipo yeye akasema. . . “Mimi niwe na raha na bwana wangu, yeye akiwa mkongwe?” Alilitilia shaka.

<sup>209</sup> Ndipo Malaika, Mjumbe, yule Mtu, Mwanadamu, katika mwili wa mwanadamu, akila ndama wa ng’ombe na kunywa maziwa yake, na kula mkate, kasema, “Kwa nini Sara akacheka, huko nyuma nyuma Yangu?” Unaona? Wazia hilo.

<sup>210</sup> Yesu alisema, “Hiyo itajirudia tena, kama ilivyokuwa.” Kufanya nini? Sasa kumbukeni, Huyo hakufanya hivyo huko chini Sodoma. Alidhihirisha tu hiyo ishara hapa juu kwa kundi teule ambao hawakuwa wanaenda kuwa motoni. Kumbukeni, hiyo ilikuwa tu kabla ya falme mashuhuri za Kimataifa zilipoteketazwa. Na hilo hasa ndilo linaloenda kutendeka sasa. Hilo ndilo tunalotazamia, sasa hivi. “Mungu,” Yesu alisema, “atadhihirishwa,” kwa maneno mengine, “katika siku za mwisho, ndani ya wanadamu. Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu.”

<sup>211</sup> Pia, kumbukeni, wateule kamwe hawakuona ishara yoyote nyingine baada ya hiyo. Hakuna wakati mmoja ambapo Mungu alimtokea Ibrahimu baada ya hapo. Hakuna kitu chochote kingine ulimwenguni, ila Sara alibadilishwa mara moja akawa msichana, naye Ibrahimu akawa kijana mwanaume; ndipo wakateremka chini, naye Abimeleki alimpenda na alitaka kumwoa, na yeye akiwa na umri wa miaka mia moja. Ndipo wakamzaa mtoto huyu. Kwa nini? Walikuwa wanamtazamia mwana aliyeahidiwa.

<sup>212</sup> Na huyo ndiye tunamtazamia leo hii, Mwana aliyeahidiwa. Basi kabla ya Mwana aliyeahidiwa kuwasili, Kanisa teule linapaswa kumwona Mungu akidhihirishwa katika mwili, akitaja siri za moyo, na kujua mambo mliyofanya. “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

<sup>213</sup> Kumbukeni, yule huko chini Bab-, huko Sodoma usiku wa leo, akiwapa ujumbe, ndugu mwema, Billy G-r-a-h-a-m,

herufi sita tu, G-r-a-h-a-m, (lake lilikuwa A-b-r-a-h-a-m), mjumbe kwa kanisa la kawaida, akilikemea kwao, hasa. Basi yeye alifanya nini? Mwujiza mmoja tu alifanya, kuwapofusha. Na kuhubiri Neno humpofusha asiyeamini. Naam, aliamini. Bila shaka, anaamini hili; lakini yeye alitumwa, akasema, kwa wale wanasiasa, kuwapiga. Na hiyo ni kweli kabisa, kwa hiyo ndiye huyo huko chini katika Babeli ya ulimwengu, chini huko katika—katika Sodoma mamboleo, akiwahubiria hayo madhehebu, akitwanga na kwenda.

<sup>214</sup> Na watu hata hawaikubali kwa unyofu. Hivi majuzi usiku, huko Los Angeles, kwenye uamsho mkuu, niliona mamia mara mamia wakija kufanya maamuzi. Vijana wakija, matineja, wakipigana makofi mmoja na mwenzake, na kutafuna chingamu, na kuvutana nywele mmoja na mwenzake, na kujifanya, wakipanda kuja kufanya uamuzi. Si ajabu ni Babeli! Si ajabu ni Sodoma! Kitu chote kiko tayari kuteketezwa.

<sup>215</sup> Mungu yupo hapa. Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nguvu Zake ni sawa leo hii kama zilivyowahi kuwa. Yeye hashindwi. Hawezi kushindwa. Yeye ni Mungu. Yeye hana budi kubaki Mungu. Kweli! “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu,” si kusikia mitambo, “kuona nguvu Zake tendaji.” Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa juma hili tunaenda kumtafuta Yeye, tunaenda kumtafuta Yeye kutembea miongoni mwetu na kutuonyesha kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

<sup>216</sup> Angalia wakati Yeye aliposulubiwa, wakosoaji wa kale, wale askari walevi wa Kirumi walitokeza na kuweka kitambaa usoni Mwake, na kumpiga Yeye kichwani, kasema, “Sasa, kama Wewe ni nabii, tabiri na utuambie ni nani aliyekupiga Wewe.” Unaona? Yeye hakumfanyia ibilisi vitimbi. Yeye kamwe hakufungua kinywa Chake na kusema neno moja. Bila shaka, Yeye alijua. Walikuwa wamepitisha kijiti, mmoja kwa mwenzake, wakasema, “Wewe tuambie ni nani aliyekupiga Wewe sasa, ndipo sisi tutakuamini Wewe.” Unaona, hao ni wakosoaji, hawakuliamini. Yeye alikuwa Nabii, lakini Yeye hafanyii watu vitimbi.

<sup>217</sup> Haya si maonyesho ya pembeni. Haya si kitu, maonyesho ya jukwaani. Ni Uwepo wa Yesu Kristo. Ni Nguvu Zake miongoni mwa watu, na sisi lazima tuingie katika Hizo kwa kilindi cha uaminifu.

<sup>218</sup> Shetani pia, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu! Ulisema Wewe ungeweza kufanya miujiza, hebu nikuone Wewe ukifanya *hili*, ama kufanya *lile*.”

<sup>219</sup> Alisema, “Rudi nyuma Yangu, Shetani. Unaona, imeandikwa,” hiyo ni kweli, “kwamba utamtumikia Bwana, na Yeye pekee ndiye utakayemwabudu.” Kwa hiyo sisi. . . Ama, “Mwabudu Bwana; Yeye pekee ndiye utakayemtumikia.”

220 Sasa tunajua kwamba Yeye ni yule yule. Sasa kama tukija usiku wa leo, tunaona sasa kama... Yesu hawezi kushindwa, kwa sababu Yeye alikuwa ni Mungu. Yeye ni Neno. Neno na Kristo ni kitu kile kile. Basi ikiwa Neno linaahidi (Neno) kwamba hili linapaswa kutendeka katika siku za mwisho, Roho wa Eliya hata anapaswa kurudi katika siku ya mwisho, hiyo ni kweli, juu ya watu, na Yeye anapaswa kugeuza mioyo ya watoto wa baba iwaelekee baba zao, Fundisho, kanuni za Biblia. Wameenda mbali katika madhehebu, shirika. Na nguvu kuu za Mungu zinapaswa kuja juu ya watu, pamoja na mkuu wa amani ambaye ataituma mioyo yao kukumbuka kwamba Yeye angali anabaki Mungu, kwamba Yeye ni Mungu. Yesu aliahidi kwamba mambo ambayo Yeye alifanya, waaminio Wake watayafanya, "Kazi nifizifanyazo."

Jamaa fulani alisema, "Loo, tunafanya! Tunafanya kazi kubwa zaidi."

221 Nikasema, "Zifanye tu kazi alizofanya Yeye. Hicho ndicho Yeye alichosema, unaona. Fanya hizo kwanza."

222 Akasema, "Vema, tunao ndugu wa kimadhehebu karibu, ambao wanahubiri Injili kote kuzunguka ulimwengu. Yeye asingeweza kufanya hivyo."

223 Nikasema, "Basi fanya kazi zile alizofanya Yeye, kwanza, ndipo tutazungumzia hilo."

224 Je! unatoa hotuba? Bali Yesu kamwe hakusema, "Enendeni ulimwenguni kote mkafundishe *hili*, ama mkafundishe *lile*." Yeye alisema, "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili." *Hubiri* ni "kudhihirisha nguvu za Roho Mtakatifu." "Ishara hizi zitafuatana nao," haiji kwa hotuba, hiyo ni kweli, unaona, "wanaoamini." Haiji kwa hotuba. Huja kwa Uwepo wa Mungu aliye hai akitembea miongoni, katika mwili wa kibinadamu, akijithibitisha Mwenyewe kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli. Yeye kamwe hashindwi kuwa yule yule. Huja rahisi sana. Urahisi Wake ndio ambao hupeleka nia ya kimwili mbali na Hilo.

225 Hilo ndilo lililowafanya wasimwamini Yesu. "Angewezaje mtu. . . Mbona, Wewe ulizaliwa katika dhambi, unawezaje Wewe kuja ukitufundisha jambo la kufanya? Sisi ni makuhani. Baba zetu walikuwa makuhani, babu zetu. Sisi, sisi tunaifahamu Biblia hiyo, ndani na nje. Na Wewe unajaribu kuja kutuambia jambo la kufanya?"

226 Yeye akasema, "Nyinyi ni wa baba yenu, ibilisi, nazo kazi zake mtazifanya." Unaona? Na, vema, jamani, hilo lilikuwa jambo la kigeni kusema kwa kundi la makasisi kama hilo.

Bali alisema, "Vema, tunaye Musa. Sisi ni. . . Tunajua."

227 Akasema, "Kama mngalimwamini Musa, mngenijua Mimi," Yeye akasema, "kwa sababu Musa alinena habari Zangu. Musa

alizingumza kuhusu siku Zangu. Na kama hamwezi kuamini maneno ya Musa, mtaniaminije Mimi?” Hakika. Kasema, “Kama hamwezi kuniamini Mimi, kama mwanadamu, basi aminini kazi ninazofanya; zinashuhudia kuwa mimi ni Nani.”

<sup>228</sup> Vema, hicho ni kitu kile kile. Roho Mtakatifu mkuu, Masihi, ule Upako, huja juu yetu leo hii, na Huo hutoa hasa Uhai Wake.

<sup>229</sup> Kama tu vile Beethoven ange—ange—angetoa Beethoven tena, kama uhai wa Beethoven uliishi ndani yangu, mbona, ningeweza kutunga nyimbo. Kama uhai wa John Dillinger uliishi ndani yangu, ningekuwa mhalifu. Kama uhai wa—wa mtu mwingine, chochote kile alichokuwa, hicho kingekuwa ndani yangu, maishani mwangu.

<sup>230</sup> Na kama Uhai wa Yesu Kristo uko ndani yako, hicho tu ndicho utakachokuwa. Unaona, hiyo ni hakika, utazifanya kazi Zake. Yesu alisema hivyo.

<sup>231</sup> Ninajua hilo ni gumu sana kwa watu ambao hawaamini mambo ya kimbinguni, na kadhalika. Na nimepitisha muda kwa mbali, marafiki, bali hebu niseme tu hili kwenu, katika kufunga tu. Usininii, usifunge moyo wako kwa hilo. Njoo, kuwa tu—kuwa tu na akili timamu, mwenye busara, unaona.

<sup>232</sup> Njoo, yasome Maandiko na uone kama mambo hayo ni kweli, uone kama hiyo ndiyo njia ambayo ulimwengu unajua kwamba Yeye alikuwa Masihi, uone kama hiyo ndiyo njia ambayo Yeye alijitambulisha Mwenyewe. Na kama Yeye alilifanya wakati ule namna hiyo kwa hizo jamii mbili za watu, zote mbili Msamaria na Myahudi maana walikuwa wanamtazamia Yeye, sasa wakati sisi tunamtazamia Yeye. Kumbukeni, walikuwa wamekuwa na maelfu ya miaka ya mafundisho, zaidi ya miaka elfu mbili, ya mafundisho kwamba Yeye alikuwa anakuja na kile Yeye angekuwa. Basi wakati Yeye alipokuja, hivyo ndivyo Yeye alivyojitambulisha Mwenyewe.

<sup>233</sup> Vema, kama Yeye akiya pia kwenye mwisho wa wakati wa Mataifa, inambidi Yeye kujitambulisha Mwenyewe kwa njia iyo hiyo, ama Yeye si yule yule jana, leo, na hata milele. Aliwapatia... Kama Yeye akiacha wakati huu wa Mataifa kuingia ndani, chini ya ufahamu wa kiakili, basi Yeye hakika aliwaumiza, unaona, kwa sababu Yeye alitenda hilo kuwaonyesha kwamba Yeye alikuwa ni hilo Neno. Na Yeye lazima afanye jambo lile lile.

<sup>234</sup> Hata ingawa walifunzwa, walikuwa ni viongozi mashuhuri wa kidini, wao, mbali kuliko kile tulicho nacho leo hii. Walikuwa ni taifa, taifa lililotawaliwa na sheria za Biblia. Walikuwa. Sisi, tunapaswa kuwa, lakini, loo, rehema, sote tunajua tuko mbali na hilo maili milioni moja. Watu wasingeweza kuishi katika siku hizo jinsi wanavyoishi sasa. Wanaume wakiwa na wanawake wanne au watano, na wake, wangepigwa mawe hata wafe. Na ninii—na mambo tunayofanya leo hii, na kujiita wenyewe

taifa la kidini! Hatuwezi kufanya hilo...ama wasingeweza kufanya hilo, hasa. Wao waliweza...Sisi tunaweza, bali wao hawawezi. Kwa sababu, pia, ilibidi wafunzwe. Kila mwanaume ilibidi atahiriwe. Ilibidi awe hivyo, la sivyo alipigwa mawe hata kufa. Kama hata alibeba mzigo kupita kiasi kwenye siku ya Sabato, alibeba wino tosha kuandika nyaraka nyingi kupita kiasi, alipigwa mawe hata kufa. Iliwabidi kuwa wa kidini. Nao waliisoma hiyo Biblia, mchana na usiku, na hata hivyo walikosa kumjua Masihi wao wakati Yeye aliposimama moja kwa moja katikati yao, wakati Biblia iliwaambia hicho hasa ndicho Yeye angekuwa.

<sup>235</sup> Sasa, jinsi tunavyojua. Kama nikisema, “Je! nina mkono?” Sijui kama *hii* itafanya kivuli au la; la, ni mwangaza mwingi kupita kiasi. Lakini unaposimama mbali na mwangaza, ukiangalia mkono wako, unaona kile kivuli kilicho. Ikiwa hujawahi kuona mkono wako ama hujawahi kujiona mwenyewe, ukiona kile kivuli chako kilicho basi unajua kile kitakachokuwa katika uhalisia, kwa sababu kinaakisi tu kile ulicho. Unaona?

<sup>236</sup> Sasa tunajua kile Kristo alichokuwa, kama kivuli, jinsi Yeye alivyojidhihirisha Mwenyewe. Unaona? Na tunajua huko nyuma kile Yeye alichofanya, sasa hakina budi kuakisiwa ndani yetu. Injili, Kristo, jinsi Yeye alivyoakisi Hiyo kule, jinsi Yeye anavyoakisi Hiyo leo hii, hiyo humfanya Yeye yule jana, leo, na hata milele. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

<sup>237</sup> Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu kwa ajili ya maombi. Sasa kila mmoja kwa uchaji tu kama uwezavyo kuwa, kwa dakika chache tu sasa.

<sup>238</sup> Ninasikitika kwamba Billy hakuweza kusambaza kadi za maombi. Ni—ninasikitika kuhusu hilo. Tutazitoa, kesho, nadhani, kwenye ibada, ama kungojea...Je! mna ibada ya asubuhi? La. Itakuwa ibada ya usiku, njoni kesho usiku yapata saa moja, saa moja na robo, na mpokee kadi zenu za maombi. Tutakuwa tukiwaombea wagonjwa, Bwana akipenda.

<sup>239</sup> Yesu Kristo ni mponyaji. Sasa kumbukeni, marafiki, hakuna mwanadamu aliye mponyaji. La. Hapana mtu aliye Mwokozi. Yesu Kristo, “Alijeruhiwa kwa makosa yako.” Kila mwenye dhambi amesamehewa kutoka kwa Yesu Kristo, lakini haitakufaidi kitu mpaka uikubali. “Kwa mapigo Yake wewe uliponywa.” Lazima uiamini sasa. “Uliponywa,” si utaponywa. Umeponywa tayari, lakini lazima uikubali. Sasa wewe amini hiyo kwa moyo wako wote.

<sup>240</sup> Labda, nilikuwa tu nikiwazia. Kwa kupitia tu, ni wangapi hapa ndani kwa kweli wanaliamini kwenye usiku wa kwanza, inueni mikono yenu, mnaamini kwamba kile nilichowaambia ni Kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

<sup>241</sup> Hebu tuombe. Hatutangojea kadi zozote za maombi. Roho Mtakatifu ni mkuu tu sasa kama Yeye alivyokuwa kama ulikuwa na kadi ya maombi. Kadi ya maombi haifanyi chochote ila kukupa. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

<sup>242</sup> Inamisheni vichwa vyenu. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Wakati mmoja, Yesu wa Nazareti. . . Kama ukiwahi kunishika nikifanya chochote kisicho cha kimaandiko, ambacho Biblia hii haisemi, unawajibika kuja kwangu, unaona, kuniambia. Yesu Kristo alisema. . .

<sup>243</sup> Wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, Yeye alikuwa anaenda ng'ambo ya bahari, ndipo Yeye akasimama. Basi njiani Mwake, kulikuwa na mtu aliyekuja Kwake, jina lake Yairo, na yeye alikuwa. . . maskini binti yake alikuwa mgonjwa sana, na alikuwa yuafa. Kusema kweli, alikufa kabla ya Yeye kufika huko.

<sup>244</sup> Na kulikuwa na mwanamke labda aliishi juu ya kilima, ambaye alikuwa amesikia habari Zake, na imani yake iliamini kweli kwamba ilikuwa, Yeye alikuwa ndiye Masihi.

<sup>245</sup> Kwa hiyo kulikuwa na wengi wa waandishi na Mafarisayo waliosimama karibu, wakisema, "Usimsikilize Mtu huyo. Mtu huyo atakuvuruga kabisa, uchanganyikiwe. Utakuwa unaacha sinagogi. Yeye—Yeye hataninii. . . Wewe, wewe hutajua kitu cha kuamini. Kamwe usimsikilize Mtu huyo."

<sup>246</sup> Bali hiyo haikumkomesha maskini mwanamke huyu. Biblia ilisema alikuwa ametokwa na damu kwa miaka mingi. Na alikuwa ametumia riziki yake yote na kuwapa madaktari. Nao madaktari hapana shaka walikuwa wamejaribu sana kumsaidia maskini mwanamke huyo, bali hawakuweza. Yeye angali alikuwa anatokwa damu, na alikuwa amedhoofika, labda anaonekana mgonjwa. Ndipo mara ghafla, alisikia. "Ni nini kelele hiyo huko chini ufukoni?"

Wakasema, "Yule Nabii kutoka Galilaya anakuja kupitia."

"Yule Yesu?"

<sup>247</sup> Unaona, *Yesu* ni jina la kawaida tu la Kiyahudi. Ninawajua watu wengi wanaoitwa Yesu. Moja kwa moja mahali ninapoishi huko Arizona, ninawajua wanaume watatu au wanne moja kwa moja kule, hata wahudumu, wanaoitwa Yesu.

<sup>248</sup> Lakini huyu ni Yesu aliye Kristo, Yule mtiwa mafuta, unaona, Mwana wa Mungu; basi huyu Nabii, Yesu, alikuwa anakuja kupitia. Mwanamke huyo alijua hilo, kwamba Yeye alikuwa nabii. Pia alijua kwamba Mungu alikuwa ni Neno, na Yeye huja kwa manabii Wake, kwa hiyo mwanamke huyo alisema, "Kama ninaweza tu kugusa vazi la Mtu huyo, nitaponywa."

249 Je! mnaifahamu hadithi hiyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Kumbukeni, alipenya kupitia kwenye umati.

250 Sasa, mtu yeyote anajua vazi la Kipalestina, lina vazi la ndani na joho, nalo hupwaya wanapotembea. Wanaume wote, wanawake, na wote, waliyavaa. Nayo huning’inia chini, na wanacho kitu kama stokingi juu ya mi—miguu yao, na kadhalika, kuzuia vumbi na kadhalika isitulie miguuni mwao. Basi wanapotembea, bila shaka, vazi hilo huzoa vumbi.

251 Na kwa hiyo walipopitia, mwanamke huyo labda ilimbidi kutambaa kuwazunguka. Na kila mtu walikuwa wanamkumbatia Yeye, “Rabi! *Nanii!*” Na wengine wao wakisema, “Vema, Yeye ni...hakuna chochote Kwake.” Hayo ni makundi yaliyochanganyikana, daima tunayo kila mahali. Lakini maskini mwanamke huyo alipenya na kugusa upindo wa vazi Lake.

252 Hilo lilikuwa ni vazi Lake la nje. Sasa, wewe, nisingehisi huo, ama wewe usingehisi kama niligusa koti lako, ama wewe uligusa langu, nalo liko juu yako. Hili vazi huru la Kipalestina, linalopwaya mbali *hivyo* kutoka kwa miguu Yake, bila shaka, kimwili, Yeye kamwe hakuhisi huo. Naye mwanamke huyo aligusa vazi Lake, akarudi nyuma, akaketi chini, ama chochote kile alichofanya.

253 Yesu alisimama, akasema, “Ni nani aliyenigusa Mimi?” Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Sasa tazama.

254 Sasa, huyo alikuwa ni Yesu jana. Na hakuna mtu aliyesema chochote, ndipo Yeye akaangalia kote kwenye kusanyiko mpaka Yeye akapata mahali imani hiyo ilipokuwa, na Yeye akamfunulia mwanamke huyo. Alisema, “Imani yako imekuokoa. Kutokwa kwako na damu kulikoma.” Je! hiyo ni kweli? “Imani yako.” Sasa, huyo alikuwa ni Yesu jana. Sasa ni, sasa Biblia ilisema...

255 Sasa ninajua wapo wahudumu wengi na wasomi mashuhuri wenye uwezo wameketi hapa. Sasa hivi Biblia haisemi, katika Kitabu cha Waebrania 3, kwamba, “Yeye hivi sasa ni Kuhani Mkuu, anayeishi daima kufanya maombezi juu ya ungamo letu”? Je! hiyo ni kweli? “Kuhani Mkuu anayeishi daima kufanya maombezi, na anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Je! hiyo ni kweli? Sasa kama ulimgusa Yeye, ungejua kwamba ulikuwa umemgusa Yeye? Angetenda vile vile Yeye alivyotenda jana. Je! hiyo ni kweli? Unaona?

256 Sasa kama ukimgusa Yeye, Yeye, si mtu mwingine; Yeye, kumgusa Yeye. Yeye ni Kuhani Mkuu, na umguse Yeye kwa hisia ya mambo ya udhaifu wako. “Bwana Yesu, mimi ni mgonjwa. Sina budi kufa, madaktari wananiambia siwezi kuishi, bali kwa njia fulani...ama nimetumia pesa zangu. Ha—hata siwezi kumudu kuenda kwa daktari.” Na chochote zaidi kile shida yako

ilicho, ama, hata, “Sijaenda kwa daktari,” chochote kilicho. Na useme, “Bwana Mungu, mimi ni mtumishi Wako.” Na kama wewe siye, useme, “Nitakuwa mtumishi Wako. Mimi, mimi ninakuamini Wewe. Kuna kitu kuhusu kile ambacho kimesomwa usiku wa leo, na kusemwa kwangu mimi, ambacho kinasikika kama Biblia. Nami nimesoma Hiyo na ninajua hiyo ni kweli. Naye mtu huyu anajaribu kuisai imani yetu hapa, akiisai imani yetu, papa hapa katika Jiji la New York, New York; na kutuambia kwamba Wewe ungali ni yule yule, kwamba Wewe hivi sasa ni Kuhani Mkuu na utafanya kazi juu ya jambo lile lile, kama ninaweza tu kukugusa Wewe. Bwana, nijalie niguse vazi Lako.”

257 Sasa ungewezaje kujua hilo? Sasa, njia ya pekee unayojua hilo, “Sasa, ninajua kwamba Ndugu Branham hanihui, na yeye ni mwanadamu tu, unaona. Yeye ni mwanadamu tu aliyesimama hapo, hayo tu. Yeye hajui chochote kunihusu. Lakini kama ninaweza kukugusa Wewe, basi Wewe nena naye na umjalie anene nami.”

258 Maana, Mungu hufanya kazi tu kupitia wakala wa wanadamu. Ni wangapi wanajua hilo? Hiyo ni hakika. Yeye kamwe hafanyi chochote nje ya wanadamu. La, bwana. “Hafanyi chochote mpaka kwanza Yeye akifunue kwa manabii Wake.” Je! hilo ndilo Biblia ilisema? Hao ni wahubiri Wake. Naam.

259 Sasa wewe amini hilo kwa moyo wako wote, na useme, “Bwana Yesu, jalia...” Sasa usiwe—usiwe mwepesi wa kushtuka, kutahamaki, unaona; wewe jipenyeze, wewe ruka juu yake, unajaribu kukifanya kitu fulani. Vema, rahisi tu.

260 Ni wangapi hapa ndani ambao ni mgeni kwangu, na ni mgonjwa? Hebu tukuone ukiinua mkono wako, useme, “Ni—ninahitaji uponyaji.” Vema, sawa, kwa kweli kila mmoja.

261 Simjui yeyote hapa, hasa, kumzungumzia, au kujua. Ninamjua huyu Ndugu Anthony aliyeketi hapa. Mimi...hiyo ni yapata...Na sasa, ndugu, ninaamini huyo ni Ndugu Tyler aliyeketi papo hapo, ninaamini. Huyo si ni Ndugu Pat Tyler? Naam. Vema. Nami nilifikiri hivyo.

262 Sasa ili tu kujua yeyote mwingine, huenda—huenda nimekuona, na wewe huenda umeniona, lakini Baba wa Mbinguni anajua simtambui yeyote kwenye wakati huu nyuma hapa ndani. Naam, ninamjua mvulana huyu anayeketi hapa akinasa kanda, maana yeye ni mmoja wa wavulana wetu wa kanda. Na nje ya hao...Baba yake hapana shaka yupo hapa mahali fulani, kwa sababu ninafikiri wako pamoja. Je! upo hapa, Ndugu Sothmann? Uko wapi? Loo, ni nyuma huko nyuma. Vema.

263 Sasa wewe mwenyewe, ninajua tunachelewa, na sisi...Nadhani tunapaswa kuwa tumeondoka hapa muda mrefu uliopita, bali hebu—hebu kidogo tu.

<sup>264</sup> Lipo jambo moja kusema chochote, na lipo jambo jingine kwa Mungu kuthibitisha kwamba ni kweli. Sasa kama nikisema kwamba una haki kuto-...La, huna haki kutokuamini hilo, kwa sababu ninalisoma kutoka kwenye Biblia, unaona. Unaona? Lakini sasa ikiwa Mungu anathibitisha hilo kuwa hivyo, basi utajua kama ndivyo ama sivyo.

Sasa katika unyenyekevu tu hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa ajili ya maombi.

<sup>265</sup> Bwana Yesu, ninajua hii ni changamoto kubwa. Ni changamoto ambayo labda si—si—sikupaswa kuitoa. Sijui. Bali nikihisi kwamba wengi wa watu hawa wamekuwa kwenye mikutano hapo kabla, wao, wao wanakujua Wewe na wanajua kwamba Wewe—Wewe uko duniani leo hii. Pia wanajua kwamba Wewe—Wewe hutimiza Neno Lako kwa kujiwakilisha Mwenyewe kupitia wakala wa binadamu. Basi, Bwana, ikiwa Wewe utanena tu hata na mtu mmoja, ama wawili, au labda watatu. Na Hilo lilisema, “Katika kinywa cha mashahidi wawili au watatu, na kila neno liimarishwe.” Lifanye angalau watu watatu hapa, Bwana, nisiowajua, kwamba Wewe utawazungumzia. Na acha waguse vazi Lako, halafu Wewe uniruhusu tu kuona ono na kujua la kusema. Jalia Roho Mtakatifu atumie midomo yangu, kama Wewe ulivyoitumia, na kwa neema sana, Bwana, mtu asiyestahili jinsi hii. Na hakuna mmoja wetu anayestahili, hakuna mmoja wetu; bali mtu fulani hana budi kulifanya, kwa hiyo ni—ninaomba, Mungu, kwamba Wewe utafanya hivyo usiku wa leo. Je! utafanya hivyo? Kusudi tu iweze kujulikana, jiji hili kubwa ambalo limewekwa kwa ajili ya hukumu, hivi punde. Ulimwengu wote, tunajua, hauwezi kudumu katika hali hii. Na huenda kuna watu hapa ambao hawatakuwepo tena, labda hiyo ndiyo sababu ninafanya hili, ninasema hili. Ninaomba, Baba, kwamba Wewe utalifanya Neno hili ambalo nimehubiri, Hilo ni Neno Lako, jalia Hilo lijulikane, katika Jina la Yesu.

<sup>266</sup> Sasa endeleeni tu kuinamisha vichwa vyenu, na mwombe tu, useme, “Bwana Yesu, jalia niguse vazi Lako.” Sasa wakati ukimaliza kuomba, basi uangalie tu huku juu, ili kwamba uweze...

<sup>267</sup> Sasa, sisemi kunitazama mimi, nyinyi nyote mnajua hilo. Kama vile Petro na Yohana walivyopita kwenye lango liitwalo Zuri, na kumwambia yule mtu aliyekuwa kiwete, “tutazame sisi,” hilo halikumaanisha...Kwa maneno mengine, “zingatia kile ninachokuambia.”

<sup>268</sup> Sasa wewe omba, na useme, “Bwana Yesu, Ndugu Branham hanijui, lakini Wewe unanijua. Nijalie tu niguse vazi Lako, maana ndiyo kwanza yeye aniambie Wewe ni ‘Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na hisia’ ya mambo ya udhaifu wangu, na kuniambia Wewe ni ‘yeye yule jana, leo, na hata milele,’

na kwamba Wewe ungetenda katika njia ile ile Wewe ulitenda wakati yule mwanamke alipogusa vazi Lako. Na hakika itaondolea mbali shaka lote kutoka kwangu, maana ni—nitajua basi kwamba Wewe ni yule yule jana, leo, na hata milele.”

<sup>269</sup> Na ndipo Maandiko yatatimizwa hasa. Tunaweza kumjua Yesu, usiku wa leo, kama tulivyomjua Yeye wakati ule. “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.” Kama nililingia na makovu ya misumari mkononi mwangu, ningekuwa... ingekuwa ni mnafiki. Usingemjua Yeye kwa hayo. Usingemjua Yeye kwa jinsi Yeye alivyovalia. Unamjua Yeye kwa Maisha Yake, hicho ndicho kilichomtambulisha Yeye kuwa Mtumishi wa Mungu, Nabii.

Sasa omba tu, na uwe na imani.

<sup>270</sup> Huyu hapa mama. Sitaki kumwambia chochote, kwa sababu mnaweza kuona kilicho shida yake. Mama aliyeketi hapa, nafikiri ndiye, anayo tezi ambayo anaiombea. Haionekani shingoni mwake. Bali unaweza kuangalia shingo yake kwa njia fulani, na, alipovuta sketi yake nyuma, inaonekana. Sikujui. Lakini kama utaamini kwa moyo wako wote, hiyo itakuacha. Naam. Ni—ni—ni—ni. . .

<sup>271</sup> Ikiwa tu uta—utakuwa tu na imani sasa, usiwe tu na shaka. Omba tu, na wewe useme, “Bwana Yesu, ninangojea kugusa vazi Lako. Jifunue Mwenyewe kwangu.”

<sup>272</sup> Unasema, “Unatazamia nini, Ndugu Branham?” Ono.

<sup>273</sup> Sasa iweni na kicho kabisa. Msininii, msisogee huku na huku, unaona, unaona, mnatatiza. Iweni tu na kicho kabisa.

<sup>274</sup> Hapa, angalia hii, tazama hapa. Huyu hapa mama papa hapa ndani, anaomba, ameketi, akiniangalia moja kwa moja. Ninaona kudondoka kwa damu. Ni katika tumbo. Analo tumbo linalotokwa damu. Ikiwa utaamini! Je! hiyo ni kweli, mama? Inua mikono yako. Mimi ni mgeni kwako. Sikujui, lakini hiyo ni kweli. Limekoma tu sasa. Imani yako!

<sup>275</sup> Ninataka kuwaulizeni, mwanamke huyo aligusa nini? Mimi simjui. Sijawahi kumwona katika maisha yangu. Ni mwanamke tu, ndiyo yote niyuayo. Unaona?

<sup>276</sup> Huyu hapa mama hapa juu kwenye mwisho wa . . . hapa nje karibu mwisho wa safu. Hapo tu nililiona likifanyika, ilionekana kama iliakisi kwa mama mwingine sasa hivi tu. Huyu ni yeye. Ana tatizo la mgongo na yeye . . . Shida fulani na mgongo wako.

<sup>277</sup> Weka mkono wako juu ya mama huyo karibu nawe, ana shida fulani kwenye mgongo wake, pia. Vema. Ni vigumu kwake kusimama na kuketi.

<sup>278</sup> Mama huyo aliyeketi karibu nawe anakuwa kipofu, huyu mwingine upande huu mwingine, anakuwa kipofu. Ninataka wewe uweke mikono yako juu yake, pia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni

kweli. Sasa amini kwa moyo wako wote, itakwisha. Sasa angalia kinachofanyika.

<sup>279</sup> Je! unaamini? Ninaona kivuli cheusi kinaning'inia papa hapa nyuma, kiko juu ya maskini mwanamke fulani. Yeye anaenda kufa; ana kansa. Unaona, Mungu asipomgusa, hana budi kufa. Nina hakika yeye ataninii... Mungu, nisaidie. Bibi Katur, kama utaamini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakufanya mzima. Je! unaamini hilo? K-a-t-u-r, kama unaamini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo anakufanya mzima. Simama, mama, na umpe Mungu sifa. Vema, unaweza kuenda nyumbani na uwe mzima. Sijawahi kumwona mwanamke huyo, maishani mwangu. Sijawahi kumwona, maishani mwangu. Yeye ni mgeni kabisa kwangu.

Unasema, "Vema, ulitaja jina lake."

<sup>280</sup> Vema, hilo si zaidi. Yesu alitaja jina la Simoni, akamwambia jina lake lilikuwa ni Simoni, kwamba baba yake alikuwa ni nani. Je! hiyo ni kweli? "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu."

<sup>281</sup> "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Hivi hamwamini hilo? Hivi hamwamini kwamba mpo moja kwa moja katika Uwepo Wake sasa? Ni wangapi wanaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Tunataka kumwona Yesu sasa, Yesu Kristo! Sasa, haikuwa ni mimi niliyewaponya watu hao. Sasa Hii hapa inaenda tena. Unaona? Vema, iweni tu na imani.

<sup>282</sup> Nawaambieni jambo mfanye sasa hivi. Nyinyi waaminio wekeaneni mikono yenu mmoja juu ya mwenzake, namna hii, mnaona, weka mkono wako juu ya mtu fulani aliye karibu nawe. Yesu, ninaenda kunukuu Maneno ya mwisho ambayo Yeye alisema wakati Yeye alipoondoka duniani, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Je! mlisema mliamini? "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

<sup>283</sup> Bila shaka, tuna imani na tuna kutokuamini, zimechanganyikana. Daima tuna hilo. Daima kuna matabaka matatu ya watu; waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini. Na sisi tuna hayo, pia. Lakini maombi yako sasa, mahali umeketi, kuwa na imani kwa ajili ya mtu huyo uliyeweka mikono yako juu yake. "Amini," Yesu Kristo alisema hili.

<sup>284</sup> Kumbuka sasa, ikiwa huamini, kuwa mwangalifu sana, maana magonjwa haya hutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine. Tunajua hilo. Tunalisoma katika Biblia, ambapo roho ovu zilitoka ndani ya mmoja zikamwingia mwingine papo hapo. Na tunaliona lote... Wengi wenu mmekuwa katika mikutano na kuliona. Kama hiyo ni kweli, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika, watu wamepooza, na kupigwa na ububu, wanakufa, papo hapo katika mkutano, kila kitu.

<sup>285</sup> Sasa katika njia ile unayoomba, wewe usijiombee mwenyewe. Wewe mwombee yule uliyeweka mikono yako juu yake. Unaona, wewe waombee.

<sup>286</sup> Na sasa ikiwa kuna mtu hapa ndani, wakati wameunganika namna hiyo, ambaye si Mkristo, na unataka kumkubali Kristo kama Mwokozi wako, naomba ufanye ijulikane kwa kusimama tu kwa miguu yako, useme, “Ninataka kumkubali Yesu kama Mwokozi wangu, sasa hivi, katika Uwepo Wake. Ninataka kusimama, kuonyesha kwa kusanyiko hili, mimi ni ushuhuda kwa Yesu Kristo. Nitamkubali Yeye sasa hivi, kama Mwokozi wangu.” Kama hujawahi kufanya hili hapo kabla, una majaliwa yako kusimama sasa. Yeye ataninii . . . Wewe msimamie Yeye sasa, Yeye atakusimamia baadaye wakati wewe—wewe uko kwenye Kizimba cha Hukumu. Kama wewe si Mkristo, ikubali sasa.

<sup>287</sup> Na nyinyi mliowekeana mikono sasa, ombeaneni kila mmoja na mwenzake. Sasa kumbuka, wanakuombea, wewe waombee. Sasa ninaenda kuomba hapa juu, pamoja nanyi, kwa ajili ya watu hawa wote.

<sup>288</sup> Mungu akubariki huko nyuma, ndugu yangu. Mungu wa Mbinguni, turehemu. Hilo ni jema sana, kitu cha kishujaa. Hivi kunaweza kuwa na mwingine angeweza kusimama, aseme . . . Yesu anakujua. “Hakuna mtu awezaye kuja . . .” Mungu akubariki, dada. Hilo ni jema.

<sup>289</sup> Hebu ona tu Uwepo wa Yesu Kristo ukija mkutanoni na kufanya hasa kile Yeye alichofanya katika Maandiko. Hiyo haiwezekani kabisa kwa mwanadamu kufanya hilo. Inahitaji Roho kufanya hilo.

<sup>290</sup> Sasa ukitaka kumwita Huyo, kama Mafarisayo, “roho mwovu,” basi utapokea tuzo hilo.

<sup>291</sup> Na kama utamwita Huyo, “Roho wa Mungu,” basi mkubali Huyo. Mkubali Yeye kama Mwokozi wako, kwa kuwa Yeye ni Yesu Kristo, ni Mwokozi pekee wa ulimwengu. Na Yeye ni—Yeye ni Mwana wa Mungu, alikufa kwa ajili yako, Yeye yupo hapa usiku wa leo katika utu wa Roho Mtakatifu. Yeye angali ni Yesu, angali ni Yesu Kristo katika utu wa Roho Mtakatifu, ambaye ni Kristo katika umbo la Roho. Na kama hujawahi kumkubali Yeye kama Mwokozi, naomba usimame tu, unajua, na Yeye atakushuhudia kama wewe utamshuhudia Yeye.

<sup>292</sup> Wengine walisimama. Iwapo kuna mwingine, upesi sana kabla hatujaomba; Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, wewe, katika Uwepo Wake. Hilo ni jema. Wengi, hilo ni jema. Mungu akubariki. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, huko nyuma, mtu huyo amesimama tayari, akainua mikono yake. Mungu akubariki. Na Mungu akubariki. Hilo ni jema. Mungu akubariki. Hilo ni ajabu. Hiyo ni kweli. Mchukue Yeye sasa hivi.

293 Kumbukeni, hivi sasa, katika Jina la Yesu Kristo, hamna maisha hapa ndani ambayo yangeweza kufichwa kwa Mungu sasa hivi, ila kile Yeye angeweza kunifunulia hakika kabisa. Mnajua hilo. Nyinyi, wengi wenu mmekuwa katika; nyinyi nyote ambao mmekuwa katika mikutano hapo kabla, na kumwona tu Huyu akifanya mizunguko mikubwa, semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika. Mnajua ni kweli. Na hivi sasa, ninajua wapo watu hapa ambao wanapaswa kujisalimisha wenyewe kwa Kristo. Tafadhali fanyeni hivyo. Tafadhali fanyeni hivyo sasa wakati nyinyi—wakati mkiwa na nafasi, katika Uwepo Wake wa Kiungu. Loo, jichunguze! Huenda tumechelewa kuliko tunavyofikiria, sasa hivi.

294 Wakati Yeye, Uwepo Wake mkuu, ukiingia na kutubariki, na kuthibitisha kwa Maandiko, Huyu hapa, Neno lililothibitishwa. Watu wanane au kumi papa hapa, wameponywa, wakiwa wameketi papa hapa. Na ni zaidi. Kama mtachukua neno langu, kama mtumishi Wake, Nuru hiyo ambayo mnaiona kwenye picha ambayo sayansi inayo papa hapa katika Washington, DC, kama “Kiumbe cha pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha,” Nuru hiyo inazunguka tu jengo hili, kuzunguka na kuzunguka, na kuzunguka na kuzunguka. Sasa, hiyo ni kweli.

295 Sasa nyinyi aminini. Yesu Kristo alisema, Maneno ya mwisho ambayo Yeye alisema wakati Yeye alipoondoka duniani, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

296 “Na Yeye alipokelewa juu Utukufuni. Ndipo wao wakaenenda kila mahali, wakihubiri, Bwana akifanya kazi pamoja nao, akilithibitisha Neno kwa ishara zilizofuata.”

297 Ombeaneni kila mmoja na mwenzake huku ninapowaombea kutoka kwenye mimbara hii.

298 Bwana Yesu, Mwana wa Mungu Yule ambaye alifufuka kutoka kwa wafu, kwenye siku ya tatu, kifo na kuzimu hazikuweza kumshikilia Yeye. Alipaa Juu, akaketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu, ambapo Yeye anaishi daima kufanya maombezi juu ya ungamo letu. Basi sasa, na Uwepo Wake muhimu hapa katika umbo la Roho Mtakatifu, ambaye amefanya kazi na kutambua mawazo yaliyo ndani ya moyo ya watu, akawaambia magonjwa yao, akawatangaza kuwa wamepona. Ee Mungu, kuona kazi Yako kuu yenye nguvu; kujua kwamba katika siku hii yenye matata, iliyochanganyikiwa, iliyojaa siasa, iliyojaa siasa za kanisa, iliyojaa kila namna ya vitu, hata hivyo Mungu aliye hai yupo papa hapa pamoja nasi usiku wa leo. Hakuna hotuba, hakuna chochote ila ushahidi, Roho Mtakatifu, moja kwa moja miongoni mwetu, Yesu Kristo akifanya mambo haya kama Yeye alivyofanya wakati Yeye alipokuwa hapa duniani. Ee Mungu, turehemu!

<sup>299</sup> Na, Shetani, unaona mikono ya watu hawa iliyowekwa juu ya kila mmoja. Wewe ni kiumbe kilichoshindwa. Huwezi kuwashikilia watu hawa tena. Ninakuapisha, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kwamba uwaachilie watu hawa na utoke ndani yao. Toka, ugonjwa na mateso, kutoka kwa watu hawa. Ninakuapisha, katika Jina la Yesu Kristo, kwamba uwaache.

<sup>300</sup> Liamini sasa kwa moyo wako wote! Kama ukiliamini, simama kwa miguu yako sasa na ulikubali. Inueni mikono yenu juu kwa Mungu, msemi, “Sasa ninakubali uponyaji wangu. Ninaamini.” Sasa inueni mikono yenu na mumpe Yeye sifa, msemi, “Asante, Bwana Yesu!” 

*BWANA, SISI TUNATAKA KUMWONA YESU* SWA63-1112

(Sir, We Would See Jesus)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumanne jioni, tarehe 12 Novemba, 1963, katika Marc Ballroom kule New York, New York, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)